# Kuimarisha Ujumuishaji, Ulinzi na Ustawi wa Watetezi wa Haki za Binadamu wenye Ulemavu



Kazi hii imeidhinishwa chini ya leseni ya Creative Commons Attribution-Noncommercial-Share Alike 4.0 International License.

Ili kuona nakala ya leseni hii, tembelea tovuti ya
http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/ ama utume barua kwa anwani hii: Creative Commons, Sanduku la Posta 1866, Mountain View, CA 9404

Waandishi
**Alice M. Nah**, Kitengo cha Sosiologia, Chuo Kikuu cha Durham
**Martin Jones,** Chuo Kikuu cha York
**Marjorie Unal,** Protection International

Msanii mchoraji
**Aitor García**

Uchoraji
**Nyotumba Bonaventure**

Tafsiri ya Kiswahili
**Peter Mwangangi**

Waratibu wa uchapishaji
**Lucrecia Cisneros Rincón, Megan Thomas et Sabina Escobar**
ISBN: 978-2-931244-33-3
EAN: 9782931244333

PROTECTION INTERNATIONAL · UNIVERSITY of York · Durham University · Sida · OAK FOUNDATION · FORD FOUNDATION

# Dibaji na Mary Lawlor

Ni furaha yangu kutambulisha mwongozo huu muhimu sana wa Kuimarisha Ujumuishaji, Ulinzi na Ustawi wa Watetezi wa Haki za Binadamu wenye Ulemavu. Katika wadhifa wangu kama Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu hali ya watetezi wa haki za binadamu, nimeangazia jinsi watetezi wenye ulemavu duniani kote wanaleta mabadiliko katika jamii zao. Katika kampeni yangu ya mwaka 2022, **Breaking Barriers**, iliyochapishwa kwa ushirikiano na Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu Gerard Quinn, niliangazia jinsi serikali na mashirika yasiyo ya serikali yanaweza kuwajumuisha watetezi wa haki wenye ulemavu katika mikutano, matukio na mashauriano. Hii inahusisha masuala kama vile kurahisisha ufikikaji katika majengo, kutoa tafsiri katika lugha ya ishara na pia maelezo ya maandishi katika video, na kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanashauriwa katika masuala mengi yanayowahusu, na sio tu kuhusu ulemavu.

Katika kutekeleza majukumu yangu, nimekutana na watetezi wa haki za binadamu kutoka sehemu mbali mbali duniani wenye jinsia, tamaduni, umri na utambulisho tofauti. Natambua jinsi mtazamo wa kila mtetezi ni wa kipekee na muhimu. Inasikitisha pia kuona jinsi watetezi wa haki za binadamu wanavyotengwa kimakusudi na pia kupitia mifumo na wale walio mamlakani ambao wanafanya maamuzi yanayoathiri maisha yao. Wanawake watetezi wa haki za binadamu hukumbwa na hatari kama vile dhulma za kijinsia, kutengwa na unyanyapaa kutokana na kukabiliana na kanuni na mitazamo inayowapendelea wanaume au mahusiano ya mwanaume na mwanamke tu.

Mwongozo huu unajumuisha tajriba na uzoefu wa watetezi wa haki wenye ulemavu ili kueleza jinsi sisi sote tunafaa kufanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha kuwa harakati za kutetea haki za binadamu zinajumuisha kila mtu. Sote tunahitaji kutambua jinsi mfumo unaofahamika kama ableism kwa kiingereza (mfumo unaokandamiza wa kutathmini uwezo na thamani ya watu kulingana na vigezo fulani, na ambao umefanywa kuwa kawaida katika jamii) unavyoathiri mahusiano, matarajio na kushiriki kwetu katika jamii. Tunahitaji kubuni na kutekeleza kanuni za ulinzi pamoja na watetezi wenye ulemavu ili kuhakikisha kuwa zinafaa katika hali na mazingira yao maalum. Tunahitaji kutathmini hatari kwa njia tofauti, tukitambua kuwa watetezi wenye ulemavu wanakumbwa na hatari kubwa na nyingi katika maisha ya kila siku.

Nakuhimiza usome mwongozi huu, ambao unaonyesha wazi jinsi harakati za kutetea haki za binadamu kote duniani zinaweza kusaidia na kuimarisha sauti, ushiriki na nguvu ya watetezi wenye ulemavu.



**Mary Lawlor**
Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu
hali ya watetezi wa haki za binadamu


# Dibaji ya Gertrude Oforiwa Fefoame

Kama Mwenyekiti wa Kamati ya Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu, nimeshuhudia na kufanya kazi na watu wengi wenye ulemavu ambao wanahusika katika juhudi za kukuza na kulinda haki za binadamu duniani kote. Huwa wanaandamana na watu waliodhulumiwa na kunyanyaswa; na huwa wanatetea wale waliotengwa au kupuuzwa. Huwa wanaangazia masuala mengi tofauti, ikiwemo haki kwa watu wenye ulemavu, haki za kijinsia, haki za afya, haki za elimu, haki za ajira, haki za jamii ya LGBTQIA+, haki za wahamiaji, waomba hifadhi na wakimbizi, usalama wa raia katika maeneo ya vita, juhudi za kuleta amani, na kadhalika.

Kama mwongozo huu unavyoashiria, watu wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto na hatari nyingi katika kutetea haki. Kuna utambulizi finyu wa suala la ableism (mfumo unaokandamiza wa kutathmini uwezo na thamani ya watu kulingana na vigezo fulani, na ambao umefanywa kuwa kawaida katika jamii) ambao huenea kwenye taasisi katika jamii. Mahitaji yao ya ufikikaji – ikiwemo kushiriki katika utetezi – yanapuuzwa kupitia mifumo iliyopo. Hili linawaacha katika hatari zaidi katika maisha ya kila siku ikilinganishwa na watu wasio na ulemavu katika jamii.

Watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu wana uwezo mkubwa wa kubadilisha jinsi haki za binadamu zinavyoeleweka na kutekelezwa. Mtazamo wao wa kipekee wa mazingira yao, ubunifu wao, jinsi wanavyokabiliana na changamoto na kutatua matatizo huimarisha jinsi jamii zinakabiliana na ukiukaji wa haki za kibinadamu na dhulma. Kwa kuunda ulimwengu ambao unajumuisha na kuthamini mchango wa watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu, tunawapa nguvu watu kutoka hulka zote uwezo na utambulizi wa kutoa mchango kwa jamii kwa njia yenye manufaa zaidi.

Mitazamo ya watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu ni muhimu iwapo tunataka kuwa na dunia yenye haki na usawa. Natumai kwamba utafurahia kusoma mwongozo huu na kupata msukumo wa kuchangia katika kujenga mifumo ya utetezi wa haki za binadamu ambayo ni jumuishi na pana, na hivyo kusaidia kuimarisha maisha ya watu wote.



**Gertrude Oforiwa Fefoame**
Mwenyekiti, Kamati ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu
Meneja wa Utetezi wa suala la Ujumuishaji wa Kijamii Duniani, Sightsavers
Rais, Baraza la Kimataifa la Elimu kwa Watu Wenye Udhaifu wa Kuona (Afrika)

# Shukrani

Mwongozo huu umechapishwa kutokana na mahojiano ya moja kwa moja na watu pamoja na makundi lengwa ya wahusika, na mazungumzo katika warsha zenye takribani watetezi 70 wenye ulemavu na wahusika katika sekta ya ulinzi kati ya 2021-2023.

Tungependa kushukuru mashirika haya kwa maoni yao kuhusu matokeo ya utafiti wa mradi huu:

**Disability Sausage Media**
**Mimi ni Mkenya (Kenya)**
**Muungano wa Wanafunzi wa Zamani wa Joytown (Kenya)**
**Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu nchini Kenya (KNCHR)**
**Mtandao wa Wanawake na Wasichana wenye Ulemavu Kenya**
**Kwa Macho (Kenya)**
**Muungano wa Kitaifa wa Wanawake wenye Ulemavu nchini Uganda (NUWODU)**
**Muungano wa Kitaifa wa Watetezi wa Haki za Binadamu, Kenya**
**Muungano wa Kitaifa wa Watetezi wa Haki za Binadamu, Uganda**
**ProtectDefenders.eu**
**Shirika la Ulemavu wa Akili (Kenya)**
**Shirika la Ugonjwa wa Kifafa Tanzania**
**Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania**
**Umoja wa Watu Wenye Ulemavu Kenya (UDPK)**
**Chama cha Kitaifa cha Viziwi Uganda (UNAD)**
**Women Challenged to Challenge (Kenya)**

Pia tungependa kutoa shukrani kwa Sarah Napoli, Perpetua Senkoro, Meerim Ilyas, na Sarah Burnard ambao walitoa maoni ya thamani katika rasimu za kwanza za Mwongozo huu, wakitueleza kuhusu tajriba na uzoefu wao katika masuala ya ulemavu na mitazamo yao katika kuwalinda watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu.

Tunamshukuru Nyotumba Bonaventure kwa kutengeneza maelezo ya michoro katika Mwongozo huu. Pia tunamshukuru Bonface Agola kwa maoni, mwitiko na usaidizi wake katika michoro hiyo.

Tunatoa shukrani zetu pia kwa msaada kutoka kwa Wakfu wa Ford, ProtectDefenders.eu, Protection International, Chuo Kikuu cha Durham, na Chuo Kikuu cha York katika kazi hii.

Makosa yote katika mwongozo huu yanasalia kuwa yetu.

Alice Nah, Martin Jones, Marjorie Unal

# Muhtasari wa Mwongozo

Kila mtu ana haki ya kukuza na kulinda haki za binadamu. Hata hivyo, watu wengi hulemazwa na muundo na mifumo ya jamii ambayo imewatenga katika kushiriki katika maamuzi yanayoathiri maisha yao. Mifumo ya utetezi wa haki za watu wenye ulemavu imekua katika nguvu na uwezo katika miaka ya hivi karibuni, ikihakiki na kukosoa jinsi mfumo unaokandamiza wa kutathmini uwezo na thamani ya watu kulingana na vigezo fulani na ambao umefanywa kuwa kawaida katika jamii umeendelea kutathmini jinsi watu huunda mazingira, miundombinu na michakato ya kufanya maamuzi.

Mwongozo huu unatathmini fasili sahihi ya watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu. Pia unaeleza kwamba watetezi wenye ulemavu wanaangazia haki nyingi, na wala sio tu haki za watu wenye ulemavu, na huenda wakakosa kujitambulisha kama 'watetezi wa haki za binadamu'. Ili kufahamu iwapo mtu ni mtetezi wa haki za binadamu, tunaangalia vitendo vyake kuona iwapo vinahusisha kukuza na kulinda haki za wanadamu.

Watetezi wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto na hatari nyingi, zikiwemo:

- Ongezeko la hatari katika maisha ya kila siku zinazohusiana na ulemavu wao
- Mkinzano wa kila siku kati ya dhana za kawaida zinazokandamiza za kutathmini uwezo na thamani ya watu kuhusu utetezi wa haki za binadamu, na matarajio kuhusu mwenendo na tabia
- Vikwazo kadhaa katika kushiriki kwao, ikiwemo vikwazo vya miundombinu, mawasiliano, kupuuzwa na ukosefu wa rasilimali.
- Vikwazo vya kijamii vinavyosababishwa na kutengwa na unyanyapaa
- Ukandamizaji na kudorora kwa mifumo ya kiraia
- Mapambano magumu na ya muda mrefu ya ujumuishaji wa haki za watu wenye ulemavu, yanayochosha na kusababisha watu kutoshiriki

Usalama wa watetezi wenye ulemavu unaweza kuimarishwa kwa kupitia:

- Kushirikisha watetezi wenye ulemavu na mashirika wanayowakilisha katika kubuni juhudi za ulinzi ili ziwe za kufaa kwa hali na mahitaji yao mahususi
- Kutathmini hatari kwa njia tofauti, kutambua kwamba watetezi wenye ulemavu wanaishi na kukabiliwa na ongezeko la hatari kutokana na hali yao
- Kupigania kubuniwa kwa sheria, sera na kanuni ambazo zinawawezesha watu wenye ulemavu kutekeleza haki yao ya kutetea haki za kibinadamu
- Kukuza na kuimarisha mtandao wa watetezi wenye ulemavu
- Kukuza 'afya njema na uzima' baina ya watetezi wenye ulemavu

Kwa jumla, ni muhimu pia kwa mifumo ya utetezi wa haki za binadamu kuhusisha zaidi na kuwajumuisha watetezi wenye ulemavu. Hii inaweza kufanyika kupitia:

- Kulipa kipaumbele suala la ushiriki wa maana na uongozi wa watu wenye ulemavu
- Kutambua na kukabiliana na mfumo unaokandamiza wa kutathmini uwezo na thamani ya watu kulingana na vigezo fulani, na ambao umefanywa kuwa kawaida katika jamii
- Kufadhili watetezi wenye ulemavu na juhudi za ujumuishaji katika mifumo ya kutetea haki za binadamu

# Yaliyomo


Dibaji na Mary Lawlor 4

Dibaji ya Gertrude Oforiwa Fefoame 5

Shukrani 6

Muhtasari wa Mwongozo 7

Utangulizi 10

Mwongozo huu ni wa nani? 10

Muhtasari wa Mwongozo 10

**1. Ulemavu na harakati za kutetea haki za binadamus 11**

1.1 Kuelewa 'ulemavu': Mbinu yenye haki kama msingi 12

1.2 Mitindo tofauti ya kukabili ulemavu: Mitindo ya kimatibabu, kijamii, na haki za binadamu 13

1.3 Kiini cha harakati za utetezi wa ulemavu: Ufahamu, ujumuishaji, haki 15

1.4 Tofauti katika makabiliano ya ulemavu 16

1.5 Adabu na itifaki za ulemavu 18

**2 Watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu 20**

2.1 Haki ya kutetea haki za binadamu 21

2.2 Watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu ni kina nani? 22

2.3 Changamoto na hatari: Maisha ya watetezi wenye ulemavu 22

2.3.1 Ongezeko la hatari katika maisha ya kila siku 23

2.3.2 Kukabiliana na mfumo wa ukandamizaji wa 'ableism' 24

2.3.3 Ufikikaji wa kushiriki katika utetezi 25

2.3.4 Vizuizi vya kijamii: Kutengwa na unyanyapaa 27

2.3.5 Ukandamizaji na kuzimwa kwa shughuli za utetezi 27

2.3.6 Mapambano ya muda mrefu ya ushirikishwaji na haki za ulemavu 29

2.4 Kuimarisha usalama na ulinzi wa watetezi wenye ulemavu 29

2.4.1 Kuhusisha watetezi wenye ulemavu na mashirika wanayowakilisha katika kubuni na kutekeleza taratibu za ulinzi 29

2.4.2 Kukadiria hatari kwa mbinu tofauti 33

2.4.3 Kutetea sheria, sera na taratibu za kuwawezesha watu wenye ulemavu kutumia haki yao ya kutetea haki za binadamu 33

2.4.4 Kuwezesha ujenzi wa mitandao na mifumo ya uanaharakati miongoni mwa watetezi wenye ulemavu 33

2.4.5 Kukuza 'ustawi katika vitendo' kati ya watetezi wenye ulemavu 35

**3 Kuimarisha ujumuishaji katika harakati za kutetea haki za binadamu 37**

3.1 Kuzingatia ushiriki wenye maana na uongozi wa watu wenye ulemavu 38

3.1.1 Kuajiri watu wenye ulemavu na kukidhi mahitaji yao kwa njia inayoridhisha 38

3.1.2 Kushirikiana na watetezi wenye ulemavu na mashirika wanayowakilisha 39

3.1.3 Kusaidia kuimarisha uongozi wa watetezi wenye ulemavu 40

3.2 Kukiri na kukabiliana na ukandamizaji uliofanywa kuwa kawaida 40

3.2.1 Kuendelea kujifunza kuhusu ulemavu na haki 41

3.2.2 Kujumuisha ulemavu katika jamii 41

3.2.3 Mpango wa kutumia njia mbili kwa pamoja 42

3.2.4 Programu, miradi na bajeti zinazojumuisha ulemavu 42

3.2.5 Kukusanya na kupanga taarifa kuhusu ulemavu 43


3.2.6 Mawasiliano jumuishi 44

3.2.7 Kuahidi na kujitolea kutekeleza ufikikaji wa kina kwa wote na muundo wa jumla 45

3.3 Kufadhili watetezi wenye ulemavu na kuwajumuisha katika harakati za haki za binadamu 46

**Mapendekezo 47**

**Marejeleo 48**



## Utangulizi

Kote ulimwenguni, watu wenye ulemavu wanahusika katika juhudi za kukuza na kulinda haki za binadamu katika njia tofauti. Huwa wanaangazia haki, usawa, kukomeshwa kwa ubaguzi, na kutekelezwa kwa haki muhimu za binadamu katika nyanja zote za maisha. Wanafanya hivyo kama watu binafsi na kwa pamoja, katika hafla za umma na zisizo za umma, wakiwa na usaidizi wa watu wengine au wakikosa usaidizi huo.

Na japo haki za watu wenye ulemavu na mifumo ya utetezi wa haki za watu wenye ulemavu zimekuwa zikikua katika miaka ya hivi karibuni, suala la hali ya watetezi wenye ulemavu na mazingira yanayowawezesha kustawi katika uhamasishaji halijapewa kipaumbele. Mifumo ya kijamii, ya kisiasa na ya kiuchumi bado inaendelea kuhakikisha kuwepo kwa mfumo unaokandamiza wa kutathmini uwezo na thamani ya watu kulingana na vigezo fulani na ambao umefanywa kuwa kawaida katika jamii, kwa viwango vikubwa na vidogo, ambavyo pia huathiri jamii za wanaharakati. Watetezi wenye ulemavu hukumbwa na changamoto za moja kwa moja na pia zisizo za moja kwa moja na hatari ambazo huzuia uwezo wao wa kukuza na kulinda haki za binadamu.

## Mwongozo huu ni wa nani?

Mwongozo huu umeandikwa kwa watu wanaohusika katika usalama na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu (‘wahusika katika ulinzi’). Unalenga kukuza uelewa wa pamoja na kuimarisha mjadala kuhusu changamoto na hatari ambazo wanaharakati wenye ulemavu hukumbana nazo na hatua ambazo zinaboresha usalama, uzima na afya yao. Wakati tulipokuwa tukifanya kazi hii, tuligundua kuwa watetezi wenye ulemavu hawawezi kulindwa kikamilifu iwapo wanatengwa na mifumo ya kutetea haki. Kwa hivyo, mwongozo huu pia unaangazia hatua za kuimarisha ujumuishaji wa masuala ya watu wenye ulemavu katika mifumo na mashirika ya kutetea haki za binadamu.

## Muhtasari wa Mwongozo

Sehemu ya Kwanza ya Mwongozo huu inatambulisha ulemavu na mifumo ya utetezi wa haki za binadamu. Inaangazia umuhimu wa jinsi tunavyoelewa ‘ulemavu’ na mtazamo wetu kuhusu watu wenye ulemavu. Inatambua ukuaji mkubwa ambao umeshuhudiwa duniani kuhusu mifumo ya utetezi wa haki katika kipindi cha miongo kadhaa. Inatathmini hatua ambazo zinaimarisha sauti, mtazamo na nguvu ya watetezi wenye ulemavu, na pia wale wanaozidunisha. Sehemu ya Pili ya Mwongozo huu inaangazia swali kuu: ‘Watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu ni kina nani’? Inaweka wazi baadhi ya changamoto na hatari kuu ambazo watetezi wenye ulemavu hupitia. Inaangazia masuala ya kipaumbele ya kuimarisha usalama, afya na uzima wao. Sehemu ya Tatu inaangazia mabadiliko pana ambayo yanahitajika ili kuimarisha ujumuishaji wao katika mifumo ya kutetea haki za binadamu.

# 1 Ulemavu na harakati za kutetea haki za binadamu

## Kuelewa ‘ulemavu’: Mbinu yenye haki kama msingi

Shirika la Afya Duniani (WHO, 2022) linakadiria kuwa kuna takribani watu bilioni 1.3 wenye ulemavu, ambayo ni sawa na asilimia 16% ya idadi ya watu duniani kote.

**Mkataba wa haki za watu wenye ulemavu (CRPD) unasema kwamba:**

> ***“Watu wenye ulemavu wanajumuisha wale wenye udhaifu wa muda mrefu wa kimaumbile, kiakili na kihisia ambao unapokumbana na vikwazo mbalimbali unaweza kuzuia uwezo wao wa kuchangia kikamilifu katika jamii kwa kiwango sawa na wengine (Kifungu cha 1).”***

Kuna tofauti muhimu kati ya udhaifu wa kimaumbile na ulemavu. **Udhaifu** wa kimaumbile ni “matatizo katika utendaji wa mwili kama vile kupungua au kupotea kwa uwezo wake kwa kiasi fulani” (WHO 2002, ukurasa wa 10). Mifano ya matatizo hayo ni kama vile kupoteza kiungo cha mwili, kupoteza uwezo wa kusikia, kuharibika kwa mfumo wa neva, hali ya afya ya akili, kusikia uchungu mkali, ugumu wa kuzungumza, shughuli nyingi kupita kiasi, na changamoto ya mwili katika kuelewa taarifa zinazotolewa na mfumo wa neva. Katika baadhi ya visa, matatizo haya hayatambuliwi kwa njia ya kimatibabu na hupuuzwa. Kila mtu hukabili udhaifu kwa njia tofauti.

**Ulemavu** nao unahusu jinsi vikwazo katika jamii humzuia mtu mwenye udhaifu katika kuchangia kikamilifu katika jamii.. kama mkataba wa CRPD unavyosema, “ulemavu hutokea pale mtu aliye na udhaifu fulani anapokumbana na vikwazo vya kimtazamo na kimazingira ambavyo vinazuia uwezo wake wa kuchangia kikamilifu katika jamii kwa viwango sawa na wengine” (Dibaji, e). Sababu za kimuktadha zinajumuisha zile za kimazingira kama vile mitazamo ya kijamii, muundo wa majengo, mifumo ya kisheria na sera, na pia sababu za kibinafsi kama vile jinsia ya mtu, umri, uzoefu na uwezo wa kukabili changamoto tofauti. Kwa jumla, jinsi jamii yetu ilivyoundwa hutathmini iwapo udhaifu wa mtu unawafanya kukosa kushiriki katika mazingira na matukio fulani – ni vikwazo katika jamii ambavyo hulemaza watu, na wala sio udhaifu au utofauti wao.

Mtazamo huu unatuelekeza kutathmini ni kwanini na jinsi mtu hufanywa kuwa mlemavu na jamii na unatufanya tuone jinsi hali hii inaweza kubadilishwa. Badala ya kuona mtu aliye na udhaifu wa kimaumbile kana kwamba yeye ndio ‘tatizo’ ambalo linahitaji ‘kutatuliwa’, tunaangazia jinsi vikwazo katika jamii huwazuia watu hao kushiriki kikamilifu katika jamii na katika siasa.

## Mitindo tofauti ya kukabili ulemavu: Mitindo ya kimatibabu, kijamii, na haki za binadamu

Kuna mitindo tofauti ya kuelewa ulemavu. Katika sehemu hii, tunaangazia mitindo mitatu maarufu zaidi, na kuangazia tofauti kuu kati yake. Mtindo wa kwanza wa kuelewa ulemavu ni **mtindo wa kimatibabu wa ulemavu**, mtindo wenye nguvu na ambao kwa jumla hukataliwa na watetezi wa haki za watu wenye ulemavu. Mtindo huu huona ulemavu kama tatizo lililopo ndani ya mtu binafsi ambalo linahitaji kurekebishwa au kutibiwa ili mtu huyo arejee kuwa wa 'kawaida'.

Katika mtindo huu, watu wenye ulemavu wakati mwingine huonekana kama watu wanaohitaji kusaidiwa na kulindwa, mara nyingi kupitia hatua za kuwatenganisha na watu wasiokuwa na ulemavu, kwa mfano, kwa kuwapeleka katika shule maalum, hospitali na taasisi maalum. Pia katika mtindo huu, watu wenye ulemavu huonekana kama watu wasiokuwa na uwezo wa kujifanyia maamuzi muhimu na hivyo wanahitaji watu wengine kuwaamulia, kama vile mlezi wa kisheria. **Mlezi wa kisheria** ni mtu aliye na mamlaka ya kisheria ya kufanya maamuzi kwa niaba ya mtu ambaye anadhaniwa kuwa hawezi kujifanyia maamuzi hayo, kwa mfano, maamuzi kuhusu makazi yao, afya na matibabu, na maamuzi ya kifedha. Mtindo huu unakosolewa kwasababu hauwapi watu wenye ulemavu sauti, fursa ya kushiriki na nguvu.

Tofauti na mtindo huu, **mtindo wa kijamii wa ulemavu** unaangazia jinsi jamii husababisha na kuimarisha ubaguzi na dhulma dhidi ya watu wenye udhaifu wa kimwili. Kama vile Michael Olive, mmoja wa waanzilishi wa mtindo huu anavyoeleza,

***...ulemavu kulingana na mtindo huu wa kijamii, ni mambo yote ambayo yanaweka vikwazo kwa watu wenye ulemavu; kuanzia kwa mitazamo hasi ya watu binafsi hadi katika ubaguzi wa kitaasisi, kutoka kwa majengo ya umma yaliyo na changamoto za ufikikaji hadi usafiri wa umma ambao hauwezi kutumiwa na watu wote, kutoka mifumo ya elimu inayotenga watu fulani hadi katika ajira zenye ubaguzi, na kadhalika. Aidha, matokeo ya kushindwa huku hayaathiri tu watu binafsi lakini kimfumo huathiri watu wenye ulemavu kama kundi ambalo hupitia hali hii ya ubaguzi ambao umefanywa kuwa kawaida katika jamii (Oliver, 1996, ukurasa. 33).***

Mtindo unaopendelewa na mashirika ya kutetea haki ni **mtindo wa haki za binadamu wa ulemavu**, ambao msingi wake ni mtindo wa kijamii wa ulemavu na zaidi ya hilo huona watu wenye ulemavu kama watu wanaostahiki haki zote za kibinadamu zilizopo. Katika mtindo huu, udhaifu wa kimaumbile unachukuliwa kama sehemu ya utofauti wa binadamu na utu; unatambua kuwa ulemavu umekuwa msingi wa utambulisho wa watu, tamaduni na ushirika wao (Degener, 2017). Udhaifu wa kimaumbile haufai kutumika kama sababu ya kumyima mtu haki zake au kumzuia. Watu wenye ulemavu wanafaa kusaidiwa ili kufurahia haki zao na kufanya maamuzi kuhusu maisha yao wenyewe; hawafai kutarajiwa kuwa watu wa kupokea tu usaidizi ambao unasalia kuwategemea watu wengine. Kwa uhakika, umuhimu wa mkataba wa CRPD ni "kukuza, kulinda na kuhakikisha upatikanaji wa haki sawa na haki zote kwa watu wote wenye ulemavu, na kukuza kuheshimiwa kwa hadhi yao" (Kifungu 1).

Kanuni muhimu katika mfumo wa ulemavu wa haki za binadamu ni kwamba "udhaifu wa kimwili hauzuii uwezo wa mtu kufurahia haki zake" (Degener, 2017, ukurasa. 43). Kama tu ilivyo kwa mtu yeyote yule, haki za binadamu haziwezi kuchukuliwa kutoka kwa mtu mwenye ulemavu. Kwa mfano, mtu mwenye ulemavu ana haki ya kutambuliwa kama mtu mbele ya sheria. Mkataba wa CRPD unatoa wito kwa serikali za kitaifa "kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata msaada wa huduma, bidhaa au vifaa wanavyohitaji

katika kutekeleza wajibu wao wa kisheria" (Kifungu 12, ibara 3), ambao unaweza kutolewa kupitia huduma za kijamii na hatua zingine.

Mkataba wa CRPD unaangazia umuhimu wa **kuwazingatia watu wenye ulemavu**, ikitaja hili kama,

> ***mabadiliko muhimu na stahiki ambayo hayaongezi mzigo usiofaa au usio na usawa kwa wote, pale unapohitajika katika kisa fulani, ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanafurahia haki zote kwa njia sawa na wengine (Kifungu 2).***

Mifano ya uzingatiaji wa mahitaji inaweza kujumuisha:

- Utoaji wa hati zilizoandikwa katika njia ambazo zinaweza kueleweka na wote, kama vile kuwa na maandishi makubwa au maandishi ya kielektroniki
- Kutoa muda wa ziada katika kutekeleza majukumu au kuhakikisha kuwepo kwa maeneo tulivu ya kazi
- Utoaji wa teknolojia saidizi, kama vile teknolojia ya kusoma maneno kutoka kwenye skrini kwa sauti au kifaa cha kufanya maneno yawe makubwa
- Kukarabati maeneo ya kufanyia kazi ofisini na nyumbani
- Kujenga maeneo ya kushukia au kupandia kwenye nyumba kama za ghorofa, vifaa vya kushikilia kwa mkono, na vyoo ambavyo vinazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu katika majengo ya umma.
- Kuweka watafsiri wa lugha ya ishara na teknolojia ya kutafsiri sauti hadi kuwa maneno moja kwa moja katika mikutano.
- Kuweka ulinzi wa ziada wakati wa shughuli za kazi kwa wale walio kwenye hatari ya kuvamiwa au kushambuliwa kwasababu ya utambulisho wao.
- Utoaji wa ratiba zinazoweza kubadilika kwa urahisi kulingana na hali, na pia chaguo la kufanyia kazi nyumbani

Mkataba wa CRPD pia unaangazia umuhimu kuwa na **muundo wa kijumla**, ambao unaelezewa katika Kifungu 2 kama,

> ***muundo wa bidhaa, mazingira, programu, na huduma ili ziweze kutumiwa na watu wote, kwa kiwango kikubwa zaidi kinachowezekana, bila haja ya kufanya ukarabati au marekebisho maalum. "Muundo wa kijumla" haufai kukosa kujumuisha vifaa saidizi kwa makundi fulani ya watu wenye ulemavu pale ambapo vifaa hivyo vinahitajika.***

Kanuni za miundo ya kijumla hufaidi sio tu watu wenye ulemavu lakini pia matabaka mbalimbali ya watu kulingana na umri, ukubwa na uwezo wao.

Sanduku 1

## Kanuni nane kuu katika mkataba wa watu wenye ulemavu (UNDESA, 2023)

Hizi ni kanuni nane kuu katika mkataba wa CRPD ambazo zinaangaziwa katika vifungu maalum:

1. Heshima kwa hadhi, na uhuru wa mtu binafsi ikiwemo uhuru wa kujifanyia maamuzi yake mwenyewe
2. Kutobaguliwa
3. Kushiriki kikamilifu na kwa njia ya maana na kujumuishwa katika jamii
4. Kuheshimu utofauti na kukubali watu wenye ulemavu kama sehemu ya utofauti na hadhi ya binadamu
5. Usawa katika nafasi au fursa
6. Ufikikaji na upatikanaji wa huduma, vifaa na bidhaa
7. Usawa kati ya wanaume na wanawake
8. Heshima kwa uwezo unaozidi kuimarika wa watoto wenye ulemavu na kuheshimu haki za watoto wenye ulemavu ili kuhifadhi utambulisho wao

## Kiini cha harakati za utetezi wa ulemavu: Ufahamu, ujumuishaji, haki

Kazi ya utetezi wa ulemavu inaweza ikaonekana kama yenye taswira tofauti, kutokea katika kujenga ufahamu kuhusu ulemavu, hadi kuhakikisha ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika jamii, kuangazia haki zao, na kuhakikisha wanapata na kufurahia haki za ulemavu. Kihistoria, mitazamo hii imekuwa ikipiganiwa na harakati tofauti katika muktadha tofauti wa kisiasa na kwa msisitizo tofauti.

**Mashirika ya watu wenye ulemavu** yana mchango muhimu katika kazi hii, ambayo imeelezewa na kamati ya CRPD katika Kauli yao ya Jumla ya 7 (2018) kama kazi inayoongozwa na mashirika, na kusimamiwa na watu wenye ulemavu, ambapo ni wazi kuwa uwingi wa uanachama wao unaojumuisha watu wenye ulemavu na ambao hukuza na kutetea haki za watu wenye ulemavu.

Harakati za ulemavu hukabili changamoto ya suala la 'ableism' katika jamii. **'Ableism'** ni ubaguzi unaotekelezwa kwa manufaa ya watu wasio na ulemavu. Mtazamo huu huwaona watu wenye ulemavu kama watu duni, wasio wa kawaida, waacha desturi na wasiopendeza. Mtazamo huu upo katika shughuli zetu za kila siku, desturi, michakato na mazungumzo, iwe tunafahamu kuhusu hili au la. Sanduku la 2 linatoa maelezo kuhusu 'ableism'.

Watetezi wa **haki za ulemavu** wanasisitiza kwamba watu wenye ulemavu wanashuhudia aina tofauti za ukandamizaji, dhulma au kutumiwa vibaya kutokana na vigezo fulani vya utambulisho wao. Kama vile mmoja wa waanzilishi wa mtazamo huu, Patty Berne, anavyoeleza:

> ***Mfumo wa haki wa ulemavu unaelewa kwamba miili yote ina upekee wake na ni muhimu, kwamba miili yote ina nguvu na mahitaji ambayo ni sharti yatimizwe. Tunajua kwamba tuna nguvu na uwezo mkubwa sio kwa sababu ya kutokuwa na upekee wa miili yetu, lakini kwasababu ya upekee huo. Tunaelewa kwamba miili yote inajipata kwenye vizuizi vinavyohusu uwezo wetu, asili, jinsia, jinsi, daraja katika jamii, taifa na ubepari, na kwamba hatuwezi kutenganisha hayo. Haya ni maeneo yanayotupa msingi wa changamoto tunazozipata (Berne, 2015).***

Sanduku 2 **Maelezo kuhusu 'ableism' (Lewis, 2022)**

Talila A. Lewis, abogada defensora de la justicia social y educadora, define el capacitismo de la siguiente manera:
*Mfumo wa kuipa miili na akili ya watu thamani kulingana na dhana zilizojengwa na jamii kuhusu ukawaida, utendaji na uzalishaji, kupendelewa na watu, maarifa, ubora na uzima. Dhana hizi zilizojengwa zimetokana na asili zenye kina kirefu kwenye masuala ya yujeniki (dhana ya kuzalisha watoto wenye afya ili kudhibiti jeni ya watu au jamii fulani), vuguvugu lisilopendelea watu wenye rangi nyeusi, chuki dhidi ya wanawake, ukoloni, ubeberu na ubepari.*
*Mfumo huu wa ukandamizaji husababisha watu na jamii kuwapa watu thamani kulingana na utamaduni wao, umri, lugha, muonekano, dini, sehemu yao ya kuzaliwa au kuishi, uzima wa kiafya, na uwezo wao wa kupata watoto kwa njia inayoridhisha na pia kufaulu katika Maisha na tabia zao.*
Sio lazima uwe na ulemavu ili kulengwa au kukabiliana na 'ableism' (Lewis, 2022).

Sins Invalid (tarehe haijulikani), shirika la haki za ulemavu, liliwasilisha **kanuni 10 za haki za ulemavu ambazo ni:**

1. **Mkingamano**
2. **Uongozi wa wale walioathiriwa zaidi**
3. **Siasa zinazopinga ubepari**
4. **Umoja wa miungano ya kutetea haki**
5. **Kutambua uzima**
6. **Uhimilivu**
7. **Kujitolea kwa mshikamano wa watu wenye aina tofauti za ulemavu**
8. **Kutegemeana**
9. **Ufikikaji wa pamoja**
10. **Ukombozi wa pamoja**

Kanuni hizi zinasisitiza umuhimu wa **mkingamano**, na kutambua jinsi vigezo tofauti vya utambulisho kama vile rangi, tabaka, jinsia, umri, dini, hali ya uhamiaji na eneo la kijiografia ni muhimu katika jinsi tunavyohisi na kukabili mapendeleo na ukandamizaji. Zinatoa wito kwa **uongozi wa wale walioathiriwa zaidi**, yaani, harakati za haki za watu wenye ulemavu ziongozwe na watu ambao sio 'wataalamu' bali ziongozwe na watu walioathirika zaidi na mifumo ya ukandamizaji ili kazi yenyewe iwe na msingi katika matatizo halisi yaliyopo na katika njia bunifu za kupinga.

Zinasisitiza umuhimu wa **umoja wa miungano ya kutetea haki**, yaani harakati za kutetea haki za watu wenye ulemavu zishikamane na harakati zingine zinazofanya kazi kutetea haki na ukombozi, pamoja na **kujitolea kwa mshikamano wa watu wenye aina tofauti za ulemavu** ili kuondoa suala la kutengwa kati ya watu wenye aina tofauti za ulemavu. Pia zinatetea ukombozi wa pamoja, zikisema:

> *"Tunasonga pamoja kama watu wenye uwezo tofauti, wa rangi mbalimbali, wa jinsia tofauti, matabaka yaliyochanganyika, katika nyanja mbalimbali, wigo mpana wa mitazamo ya mahusiano ya kingono, tukiwa na maono ambayo hayaachi mtu yeyote nyuma." Sins Invalid (mwaka haujulikani).*

## Tofauti katika makabiliano ya ulemavu

Njia ambayo kila mtu hukabiliana na ulemavu wake ni ya kipekee na inategemea mambo kama vile ukubwa wa udhaifu wake wa kimaumbile, jinsi udhaifu huo unavyoingiliana na viungo au vipengele vingine vya mwili na utambulisho wake, na njia ambazo udhaifu wake unavyoeleweka, kukubalika, na kushughulikiwa katika muktadha wa jamii zao. Kama vile mwanamke mmoja mtetezi anayekabili kupoteza uwezo wa kusikia alivyotuelezea:

> ***Ulemavu unachanganya, unavuruga, na una utofauti – kiwango changu cha kupotea kwa uwezo wa kusikia si sawa na kiwango cha kupotea kwa uwezo wa kusikia kwa mtu mwingine - kuna tofauti nyingi katika jinsi kila mtu anavyoingiliana na ulemavu ambao ni wa aina sawa ama aina tofauti.***

Kwa hivyo, hatuwezi kudhani kuwa watu walio na aina fulani ya ulemavu (k.m. ugonjwa sugu unaodumu muda mrefu) wana matukio na hisia sawa katika maisha, na hatuwezi kudhani kuwa mahitaji waliyonayo ni sawa.

Watu wengi hawajioni kama watu wenye ulemavu ingawa wanaweza kutimiza vigezo vya mtu kuwa na ulemavu. Katika mradi huu, watetezi kadhaa wenye ulemavu walitueleza kwamba huwa wanaanza kujitambua kama 'watu wenye ulemavu' wanapojifunza zaidi kuhusu suala la ulemavu. Kama vile mtetezi mwanamke mwenye ulemavu alivyoeleza katika mahojiano,

> ***… kutambua ulemavu wangu na kufikia uwezo wa kuutaja… ulichangiwa na mtandao wa wanawake niliokuwa nao, na kukutana na wanawake wengine wenye ulemavu ambao walinisaidia kujua jinsi ya kuuelezea.***
>
> ***Na pia, kutoona aibu wakati unapouliza kuhusu kutimiziwa mahitaji yako; kulifanya kuwa suala la kisiasa, kuelewa ni wapi kazi yako inahitaji***



*kukomea, na jinsi ya kujilinda katika kazi hiyo inayoendelea ya kuomba kutimiziwa mahitaji.*

*Kwa hivyo, nadhani suala la kisiasa lilianza nilipoingia katika mitandao ya watu wanaotetea haki na usawa kwa wanawake…*

Baadhi walielezea suala hili la kujitambua kama safari pana ya utambuzi wakati walipofahamu zaidi kuwahusu wao wenyewe, utendaji wa mwili wao, mahitaji, na jinsi ya kujitetea na kutetea watu wengine kuhusu ulemavu. Waliangazia jinsi ilivyokuwa rahisi **kuelewa na kukubali 'ableism'** wao wenyewe, kwani kila mara waliona matarajio ya jamii kuhusu urembo na kuwa na 'mwili kamilifu usiokuwa na kasoro'. Hali hii inaweza kusababisha watu wenye ulemavu kujionea aibu; inaweza kupunguza kujithamini kwao na kusababisha watu wenye ulemavu kukosa kutoa ombi la kutimiziwa mahitaji yao.

Aina nyingi za ulemavu **sio bayana** (au **hazionekani kwa urahisi**). Yaani, mtu anaweza kuwa na ulemavu ambao sio bayana kutokana na muonekano wao. Wengine wana **ulemavu unaobadilika**, yaani, mahitaji na uwezo unabadilika baada ya muda, sawia na mahitaji yao. Kwa mfano, mtu ambaye hupatwa na maumivu makali ya kichwa anaweza kuwa na siku ambazo hasikii uchungu na kuna siku zingine ambapo uchungu ni mwingi sana.

Watu wengi wana **ulemavu wa aina nyingi**. Kwa mfano, mtu anaweza kuwa na tatizo la kimatibabu (kama vile kisukari, pumu, kifafa, na uchovu unaodumu kwa muda mrefu), au ulemavu wa kisaikolojia (kama vile msongo wa mawazo, skizofrenia, mfadhaiko wa baada ya kiwewe, au wasiwasi), na ulemavu wa kiakili, utambuzi au wa ukuaji (kama vile usonji, na matatizo ya kusoma vizuri au kutambua hisia).

Mifumo inayoingiliana ya ukandamizaji hutathmini jinsi watetezi wenye ulemavu wanavyochukuliwa kwa sababu ya vipengele vya utambulisho wao, kama vile jinsia yao, kabila, elimu na tabaka. Kwa mfano, msichana wa kiasili mwenye ulemavu wa akili katika jamii ya vijijini hukabiliana na ulemavu kwa njia tofauti na mwanamume mwenye ulemavu ambao unaonekana kirahisi anayetokea katika familia inayojiweza kiuchumi. Huenda ulemavu wa yule msichana usitambuliwe na anaweza kukosa kupata usaidizi anaohitaji shuleni. Huenda yule mwanaume naye aweze kununua vifaa anavyohitaji ili kumsaidia kushiriki kikamilifu katika jamii. Kama ilivyoelezwa hapo juu, mtazamo unaolenga mkingamano wa vipengele kadhaa unaweza kufichua jinsi kila mtu anakabiliwa na ulemavu tofauti kulingana na utambulisho wao, hali na mazingira.

## Adabu na itifaki za ulemavu

Watu wasio na ulemavu wanaweza kuhisi fedheha na kutokuwa na uhakika kuhusu jinsi ya kuishi na watu wenye ulemavu. Huenda wasijue ni nini kinachofaa au maneno wanayofaa kusema au mambo ya kufanya. Kwa sababu suala la 'ableism' limejikita sana katika jamii na hutathmini jinsi watu wanavyowasiliana, baadhi ya maneno ambayo watu wasio na ulemavu hutumia katika mazungumzo ya kila siku yanaweza kuwa ya kutusi au kuwaumiza watu wenye ulemavu, kwa mfano, misemo hii ya kiingereza yenye tafsiri ya moja kwa moja kwa Kiswahili kama vile 'fall on deaf ears' (maneno yaliangukia masikio ya viziwi), 'turn a blind eye to' (kufumbia macho yaliyopofuka kwa jambo fulani ), na 'needing a sanity check' (kuhitaji uchunguzi wa akili timamu).

Suala la lugha inayofaa pia ni la kimazingira na kimuktadha – kwani kile kinachokubalika kwa mtu mmoja mwenye ulemavu kinaweza kuwa hakifai kwa mtu mwingine.

Kuna vidokezo kadhaa muhimu kuhusu **adabu na itifaki za ulemavu**, ambavyo ni, jinsi ya kushiriki na watu wenye ulemavu kwa njia ya heshima. Judy Cohen (tarehe haijatajwa) anapendekeza kanuni muhimu zifuatazo:

- Usidhani kwamba mtu mwenye ulemavu anahitaji msaada – unafaa kutoa msaada pale tu ambapo mtu anaonekana kuuhitaji, na unafaa kuuliza jinsi unavyoweza kusaidia kabla ya kuchukua hatua.
- Kuwa mwangalifu kuhusu kumgusa mtu, tambua kwamba huenda hawataki miili yao au vifaa vyao kuguswa
- Zungumza moja kwa moja na mtu mwenye ulemavu, na wala sio mtu anayeandamana naye, msaidizi, au mkalimani wake, ukiheshimu usiri na faragha yao kuhusu ulemavu wao.
- Majibu yako kuhusu maombi yao ya kutimiziwa mahitaji yawe yenye kuzingatia,

badala ya kutafsiri maombi hayo kana kwamba ni malalamiko.

- Usijifanyie maamuzi kuhusu kile wanachoweza kufanya au la, na usiwafanyie maamuzi kuhusu iwapo wanaweza au hawataweza kushiriki katika shughuli fulani

Pia anatoa ushauri huu kuhusu lugha unayotumia:

- Tangulia kwa kumtambua mtu mwenyewe kwanza kabla ya ulemavu wake, kwa mfano, kusema "mtu mwenye ulemavu" badala ya "mlemavu", na kuwauliza watu kuhusu wanapendelea kutambuliwa vipi.
- Epuka maneno yaliyopitwa na wakati kama vile "mlemavu" au "kilema" na pia maneno ya tasifida, kwa mfano maneno haya ya kiingereza yenye tafsiri ya moja kwa moja kwa Kiswahili kama "physically challenged" (changamoto za kimaumbile) na "differently abled" (aliye na uwezo tofauti)"
- Sema "mtumiaji wa kiti cha magurudumu" badala ya "kulazimika kukaa kwenye kiti cha magurudumu", ukitambua kuwa kiti cha magurudumu humkomboa mtu badala ya kumfunga mtu huyo.
- Kutumia nahau kama vile "ilikuwa vyema kukuona" au "nitakuona baadaye" kwa mtu mwenye ulemavu wa kutoona inakubalika.
- Viziwi na ambao wanawasiliana kwa lugha ya ishara wanaweza kuchukizwa au kuhisi kukosewa ikiwa utawataja kama "watu wenye udhaifu wa kusikia" kwa sababu wanajiona kuwa sehemu jamii ya watu walio wachache kitamaduni na pia kiisimu.
- Epuka maneno hasi, na ya kukatisha tamaa kama vile "mwathiriwa" au "mtu anayeteseka"

Katika mwongozo wake, Adabu na Itifaki za Ulemavu, anatoa mwongozo zaidi kuhusu mawasiliano ya heshima na watu wenye aina tofauti za ulemavu, ikiwa ni pamoja na watu wanaotumia viti vya magurudumu au wenye changamoto ya mwendo kutoka sehemu moja hadi nyingine, watu wenye ulemavu wa akili, na watu wenye ulemavu wa utambuzi wa hisia. Vidokezo hivi vinahitaji kutathminiwa kulingana na matarajio ya watu wenye ulemavu, ili kuona uhusiano na umuhimu wao.



# 2 Watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu

## Haki ya kutetea haki za binadamu

Kila mtu ana haki ya kukuza na kulinda haki za binadamu. Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Kibinadamu la mwaka 1998 (lililojulikana rasmi kama Azimio la Haki na Wajibu wa Watu Binafsi, Vikundi na Asasi za Jamii za Kukuza na Kulinda Uhuru wa Msingi na Haki za Kibinadamu Zinazotambuliwa Kote Duniani) linathibitisha haki hii, likisema:

> ***Kila mtu ana haki, kibinafsi na kwa kushirikiana na wengine, kukuza na kujitahidi kulinda na kutekeleza haki za binadamu na uhuru wa kimsingi katika ngazi za kitaifa na kimataifa.***

Watu wanakuza na kulinda haki za binadamu kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, wanafanya hivyo kwa: kuzungumzia masuala ya kijamii na kisiasa; kuangazia matukio ya ubaguzi na ukosefu wa usawa; kuzingatia matukio ya vurugu na dhulma; kutoa huduma kwa jamii zilizotengwa, kama vile msaada wa kisheria, elimu, na huduma za kiafya; kuokoa watu kutoka hali hatari; kufuatilia maeneo ambayo watu wanazuiliwa (kama vile magereza) ili kuhakikisha kwamba wanashughulikiwa kwa njia yenye utu; kufanya kampeni kuhusu sheria, sera, na hatua za serikali za kulinda haki, na kadhalika.

Ingawa kila mtu anapaswa kuwa na uwezo wa kukuza na kulinda haki za binadamu kwa njia salama, shughuli hizi zinaweza kuwa hatari. Baadhi ya watetezi hutishiwa na kushambuliwa kwa sababu ya kazi yao. Kwa mfano, wanaweza kuaibishwa hadharani au mtandaoni, kutishiwa kwamba watashambuliwa, au maisha yao binafsi kufuatiliwa kwa nia ya kuwadhuru. Wengine wamepigwa, kufanywa wahalifu, wamefungwa jela, na hata kuuawa au kutoweka. Vitisho na mashambulizi wanayokabiliana nayo hutegemea masuala kama vile mambo wanayopigania, utambulisho wao na aina ya ushirikiano wao kijamii, nia na matendo ya wakosaji wanaotekeleza uhalifu, na muktadha wa kisiasa, kijamii na kiuchumi katika maeneo wanayoishi (Nah, 2021).

Katika miaka iliyopita, wahusika muhimu wa serikali na wasio wa serikali wamekuwa wakiunda **mfumo wa ulinzi wa kimataifa kwa watetezi wa haki za binadamu walio hatarini**, unaolenga kuwawezesha kukuza na kulinda haki katika hali salama na njia zenye utu (Bennett na wengine, 2015). **Wahusika hawa wa ulinzi** hujihusisha katika shughuli mbalimbali zinazolenga kujenga mazingira salama na wezeshi kwa ajili ya utetezi wa haki, pamoja na kukabiliana na hali ya watetezi wa haki za binadamu wakati wa dharura. Shughuli zao zinajumuisha utetezi wa sheria, sera na hatua zinazotambua na kulinda haki ya kila mtu ya kutetea haki za binadamu; kukemea kutoadhibiwa kwa uhalifu dhidi ya watetezi wa haki za binadamu; na kuwapa watetezi wa haki za binadamu mafunzo ya usalama, misaada ya dharura, uhamisho wa muda, na aina nyinginezo za usaidizi, ili waweze kuwa salama wakati wanapoendeleza juhudi za kukuza na kulinda haki.

## Watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu ni kina nani?

Mtetezi wa haki za binadamu mwenye ulemavu ni mtu yeyote mwenye ulemavu anayekuza na kulinda haki za binadamu.

Watetezi wenye ulemavu hawazingatii tu haki za ulemavu, bali wanazingatia aina zote za haki na uhuru wa binadamu, kama vile haki za mazingira, haki za ardhi, haki za ajira, haki za wanawake, haki za LGBTIQA+, mabadiliko ya tabianchi, haki za mpito na mabadiliko, haki za kiuchumi, na kadhalika.

Matukio ya kukabiliana na ulemavu yanaweza kusababisha mtu kuwa mwanaharakati, na ulemavu unaweza kupatikana kupitia uanaharakati. Kufafanua zaidi, watu wenye ulemavu wanaweza kutetea mabadiliko ili wao na wengine kama wao wafurahie haki ambazo wamenyimwa. Baadhi ya watu pia hupata ulemavu kwa sababu ya uanaharakati wao, kwa mfano, wanaweza kupata madhara ya kimwili, kisaikolojia, au kiakili kutokana na matukio ya unyanyasaji, vurugu, unyanyapaa, na uhalifu, ambayo huwasababisha kuwa na ulemavu.

Watu wengi, wakiwemo wale wenye ulemavu, hawajioni kama 'watetezi wa haki za binadamu'. Wanaweza kujieleza kwa njia nyinginezo, kwa mfano, kama mwanaharakati, mtetezi, mfanyakazi wa huduma za kijamii, mwanafunzi, mwalimu, mwandishi wa habari, mlezi, rafiki anayejali, au jamaa kwenye familia. Katika baadhi ya jamii, neno 'mtetezi wa haki za binadamu' limekuwa likitumika kwa muktadha wa kipekee sana, kwa mfano, kuwatambulisha wanaharakati wenye hadhi ya juu, mashuhuri, na wala sio katika kutambulisha safu kubwa ya watu ambao wanaweza kufaa kutambuliwa kama watetezi wa haki za binadamu. Katika jamii nyingi, watu hawafahamu neno 'mtetezi wa haki za binadamu'.

Watu wengi wanaokuza na kulinda haki za binadamu hawatumii msamiati wa haki za binadamu kuelezea kazi zao. Wanaweza kuzungumzia kazi zao kwa majina tofauti, kama vile kazi ya haki ya kijamii, usawa, ushirikishwaji, utofauti, juhudi za kujenga amani, harakati za kibinadamu, au maendeleo ya jamii. Ili kufahamu kama mtu ni mtetezi wa haki za binadamu, tunaangalia matendo yake ili kuona kama yanahusisha kukuza na kulinda haki za binadamu, badala ya kile wanachojiita au vile wanavyotambuliwa na wengine.

## Changamoto na hatari: Maisha ya watetezi wenye ulemavu

Watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto na hatari katika kukuza na kulinda haki kwa hali ambayo inaweza kuwa tofauti na ile inayowakumba watetezi wasio na ulemavu. Kile ambacho hakionekani kuwa hatari kwa mtu asiye na ulemavu kinaweza kuwa hatari kwa mtu mwenye ulemavu. Baadhi ya changamoto na hatari hizi ni za **moja kwa moja** - yaani, zinawalenga watetezi wenye ulemavu. Baadhi **si za moja kwa moja** - na, zinatokea wakati sheria, sera, na desturi zilezile zinatumika kwa kila mtu kwa njia sawa lakini zinakuwa na athari mbaya zaidi kwa watetezi wenye ulemavu.

### Ongezeko la hatari katika maisha ya kila siku

Watetezi wenye ulemavu hukabiliwa na hatari katika shughuli za kila siku ambazo watu wasio na ulemavu hawakabiliani nazo. Kulingana na aina na ukubwa wa ulemavu wao, wanakumbana na changamoto na hatari zinazotokana na maeneo ambayo hayajaundwa vizuri, kukabiliwa na magonjwa ya kuambukiza ambayo yanadhoofisha zaidi afya zao (ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa virusi vya korona UVIKO-19), mbinu za mawasiliano zinazowatenga, kutengwa

kwa jamii, na kutengwa kisiasa. Kwa mfano, kutembea katika mitaa iliyojengwa vibaya na yenye msongamano mkubwa wa magari ni hatari zaidi kwa mtu ambaye ana ulemavu wa kutoona. Utanganamo katika kijamii wakati wa janga ni hatari zaidi kwa mtu ambaye hana kinga dhabiti mwilini kukabilina na ugonjwa huo. Ni lazima watetezi wenye ualbino wafanye kazi kwa tahadhari katika maeneo ambayo wako katika hatari ya kufanyiwa madhara, kutekwa nyara, au kuuawa, kwa sababu ya uchawi na matambiko ya kitamaduni. Katika baadhi ya maeneo, watetezi wanawake wenye ulemavu huzuiliwa nyumbani na familia zao, hali inayowazuia kushiriki katika harakati za utetezi.

Kwa sababu wanakabiliana na changamoto na hatari zaidi katika maisha ya kila siku, watetezi wenye ulemavu ambao tuliwahoji walipendelea kujiepusha na aina hatari za uanaharakati - shughuli ambazo zina uwezo mkubwa wa kuwaweka katika hatari na madhara. Athari za shughuli hatari zinaweza kuwa kubwa zaidi kwa watu wenye ulemavu; na wanaweza kuwa na rasilimali chache za kupunguza hatari hizi. Kwa mfano, watetezi kadhaa walizungumzia jinsi walivyoepuka mikutano na matukio ya kukuza haki za LGBTQIA+, na maandamano, wakihofia jinsi wangekwepa ikiwa polisi wangeamua kuwatawanya kwa fujo. Kama mtetezi mmoja mwenye ulemavu alivyoeleza, "Kuna kiwango cha kujilinda wewe mwenyewe na kutafuta njia mbadala za kufanya utetezi."

Watetezi wenye ulemavu katika utafiti huu pia walizungumza kuhusu **hatari za kihisia** wanazokabiliana nazo kwa sababu ya kutetea haki zao. Wako katika hatari ya kutengwa na vikundi kadhaa katika jamii, kupoteza marafiki, kukosolewa kwenye mitandao ya kijamii, kuonekana kama "mtu mgumu", na kadhalika. Kama mtetezi mwanamke mwenye ulemavu alivyoeleza kwa masikitiko, "watu husema kwamba ninalalamika sana, kwamba nina hasira sana". Hasara kama hizo zinaweza kuwa na athari kubwa kwa wale ambao tayari wanapitia changamoto za kutengwa kwa sababu ya ulemavu wao.

Hatari ambazo watetezi wenye ulemavu wanakabiliana nazo pia zinategemea jinsi wanavyoathiriwa na mifumo mingine ya ukandamizaji. **Wanawake watetezi wa haki za binadamu** hupitia hatari za ziada na tofauti kwa sababu ya jinsia yao (Forst, 2019). Kwa vitendo vile vile ambavyo wanaume wanasifiwa kwa kuvifanya, wanawake wanaweza kushutumiwa kwa kuvifanya. Wanawake mara nyingi huchukuliwa kuwa 'wanyonge' na 'waathiriwa' wanaohitaji ulinzi, badala ya kuchukuliwa kama mabingwa wanaotetea na kuleta mabadiliko. Mkingamano wa kijinsia, ukoo, tabaka, elimu, umri, utambulisho wa mtu kuhusu mahusiano ya kimapenzi na jinsia tofauti, utambulisho wa kijinsia, na vigezo vingine ni muhimu katika jinsi mtu anavyokabiliana na hatari. Katika utafiti huu, mtetezi mmoja mwenye ulemavu anayejitambua kama 'queer' (utambulisho wa kijinsia na mahusiano ya kimapenzi ambao sio 'wa kawaida') alieleza jinsi alivyokabiliana na hatari zinazohusiana na utambulisho wake wa kijinsia na vile vile hatari zinazohusiana na ulemavu wake, na haya yote yaliathiri afya yake ya akili na uzima wake kwa jumla.

## Kukabiliana na mfumo wa ukandamizaji wa 'ableism'

Watetezi wenye ulemavu ni sharti wakabiliane na mfumo uliofanywa kuwa kawaida na unaokandamiza wa kutathmini uwezo na thamani ya watu kulingana na vigezo fulani yaani 'ableism' katika maeneo ambayo wanakuza na kulinda haki za binadamu. Kama vile Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu hali ya watetezi wa haki za binadamu, na Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu watu wenye ulemavu walivyosema, watetezi wenye ulemavu "mara nyingi hulazimika kutetea haki katika mazingira na michakato yenye kukandamiza, kwa kufanya kazi na washikadau ambao hawaelewi, au hawako tayari, kutoa rasilimali kwa ajili ya

kutimiza mahitaji stahiki na yanayofaa" (Lawlor na Quinn, 2022).

Kama ilivyoelezwa hapo juu, jinsi tunavyofasili 'harakati za kutetea haki za binadamu' inaweza kuonyesha upendeleo unaowiana na mfumo wa ukandamizaji wa 'ableism'. Ni imani ya wengi kwamba hatua zote za kukuza na kulinda haki za binadamu lazima zifanyike hadharani, ziwe za mabishano, zenye utata, na zihusishe shughuli zenye hatari kubwa. Katika utafiti huu, baadhi ya watetezi wenye ulemavu wanasema wao huamua kujihusisha na **uanaharakati usiokuwa wa moja kwa moja**, kile ambacho msanii Samet Durgun (2023) anafafanua kama: "Aina ya utetezi wa chini kwa chini ambao polepole huathiri mioyo na akili za watu bila kusababisha mshtuko, dharura, au usumbufu." Kama anavyosema, "Njia hii inaweza kukosa 'kuonekana' au kutambuliwa hadharani, lakini kina cha mizizi yake kinaweza kuleta mabadiliko ya kudumu baada ya wakati fulani". Kama mtetezi mmoja mwenye ulemavu alivyosema katika mahojiano,

> ***"kwa watu kuona tu jinsi unavyofanya mambo yako, au jinsi unavyoishi na kujichukulia, jinsi unavyojibu masuala tofauti, huo bado ni utetezi ... ni 'utetezi wa kupitia utoaji mfano' - kwa jinsi unavyoishi na kufanya mambo yako."***

Mtu anaweza kukuza na kulinda haki za binadamu kupitia maneno yake na mtindo wake wa kimaisha; kupitia uamuzi wake wa kupinga ubaguzi hata wakati ambapo kuna pingamizi na vizuizi; kupitia juhudi za kila siku za kubadilisha mitazamo ya wale wanaomzunguka. Ni muhimu kutambua njia kamili ambazo watu hutetea haki za binadamu, kwani ufafanuzi finyu unaweza kusababisha kutengwa kwa watetezi wenye ulemavu ambao huchukua hatua ya kubadilisha jamii katika njia za kipole, tulivu, na zisizoonekana.

Njia nyingine ambayo dhana ya mtu kuwa na uwezo hujitokeza katika jamii za watetezi wa haki za binadamu ni **matarajio kuhusu tabia na mwenendo**. Mara nyingi wale wanaoweza kwenda kwa urahisi, kuwasiliana vizuri, kufikiria kwa haraka, na wanaoweza kutangamana vizuri na kukamata hisia za hadhira ndio hupewa kipaumbele. Matarajio hayo hufanya iwe vigumu kwa watetezi wenye ulemavu kushiriki kikamilifu. Akielezea jinsi alivyohisi wakati akisimamia mikutano, mtetezi mwanamke kiziwi alisema katika mahojiano kwamba:

> ***Watu ambao wanajihusisha na utetezi, kwa ujumla - angalau kutoka kwa mtazamo wa kiutambuzi na wa maneno - wanaonekana***



*kuwa na changamoto chache. Kwa watu ambao hawawezi kusikia au kuona... inaweza kuwa kikwazo sana katika suala la jinsi tunavyochangia, kusimamia na kusaidia katika mikutano na ni kwa njia gani tunaweza kufanya hivyo. Je, tunapandaje kwenye jukwaa wakati ambapo watu wanaweza kukosa kutuelewa?*

*Nina changamoto pale ninajaribu kuchangia katika mikutano. Lakini ikiwa mahitaji yangu hayatimizwi kupitia kwa microfoni au vitu vingine, basi sitangamani na watu wanaoshiriki kwa njia sawa, na mimi hujitenga tu... vitu vya aina hii huwa vinanizuia sana. Kwa hivyo, wakati mwingine mimi husimama na kusema, "Ninatakaje kuingia katika nafasi au tukio hilo?" Kwa sababu najua nitajipata nikikabiliwa na vizuizi...*


## Ufikikaji wa kushiriki katika utetezi

Watetezi wenye ulemavu mara nyingi hukabiliana na changamoto katika kufikia maeneo, watu, na mazungumzo ambapo wanaweza kuwasilisha masuala yao. Katika baadhi ya matukio, wao - pamoja na watu wasio na ulemavu – hukutana na vizuizi vya kimfumo katika hatua za kushiriki. Kwa mfano, wanaweza kukosa kujulishwa kwamba kuna mkutano muhimu unaofanyika, au ikiwa watafahamishwa kuhusu hilo, hawapewi kibali cha kushiriki. Pia kuna vigezo vya ufikikaji ambavyo vinahusiana haswa na ulemavu.

Cha kwanza ni **ufikikaji wa kimwili.** Hii inamaanisha kuwa na uwezo wa kufikia eneo halisi ambapo wangependa kushiriki. Hii inahusiana na muundo wa eneo hilo na miundombinu inayoathiri jinsi wanavyosafiri kwenda kwenye mkutano, kuuhudhuria na kurudi nyumbani. Kwa mfano, mtetezi anayetumia kiti cha magurudumu atapata hawezi kufikia sehemu ambayo inahitaji matumizi ya ngazi kwenye gorofa. Magari yaliyoundwa kwa matumizi ya viti vya magurudumu, vifaa vya kushikilia wakati wa kupanda na kushuka zenye muinuko unaofaa, na njia wazi na pana za kutembelea kuanzia mwanzo hadi mwisho wa safari zao zinaweza kuongeza na kuimarisha ufikikaji. Watetezi ambao wako mbali au katika maeneo ya vijijini, watapata shida zaidi kufikia maeneo ya kufanyia maamuzi.

Pili ni **ufikikaji wa kimawasiliano**. Hii ina maana ya mtu kuwa na uwezo wa kupokea, kuelewa, na kuwasiliana kwa wakati ufaao ili aweze kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi. Mtetezi mwenye udhaifu wa kusikia atakuwa na ugumu wa kuzungumza katika katika chumba chenye kelele nyingi. Eneo lililo na vifaa maalum vya kusaidia kusikia vinaweza kuongeza ufikikaji kwake. Mtetezi ambaye ana ulemavu wa kiakili atapata changamoto za ufikikaji ikiwa anapewa hati ambazo ni tatanishi na zilizojaa maneno magumu, zilizopangiliwa vibaya, hasa anapopewa hati hizo muda mchache tu kabla ya mkutano kuanza. Hati ambazo zinasomeka kwa urahisi na ambazo hazina maneno magumu, zilizopangiliwa vizuri na zinazotolewa mapema zingemsaidia kujitayarisha ipasavyo kwa mkutano huo. Baadhi ya watetezi wanaweza kuhitaji maneno kuchapishwa yakiwa makubwa, Breli au mfumo wa maandishi yenye vidutu yanayotumiwa na watu wenye ulemavu wa kutoona, mpangilio mzuri unaojumuisha rangi tofauti au hati zinazoweza kusomwa vizuri na vifaa wezeshi katika kompyuta kwa manufaa ya mtu mwenye ulemavu wa kutoona.

Tatu ni **ufikikaji unaohusu uwakilishi**. Hii inamaanisha kutambuliwa na kuonekana kama mtu anayefaa kushiriki - yaani, kutofukuzwa, kupuuzwa, au kutengwa. Muungano wa Kimataifa wa Walemavu (2020) unasema kuwa baadhi ya watu wenye ulemavu huachwa nje zaidi kuliko wengine katika mashauriano na michakato ya kufanya maamuzi, hasa wale wenye ulemavu wa kisaikolojia, ulemavu wa kutoona na pia viziwi, wanawake wenye ulemavu, pamoja na watu wa jamii asilia wenye ulemavu. Ikiwa watu wenye ulemavu




wanaonekana kuwa hawawezi kujisimamia na kujitetea na pia kutetea wengine, watatengwa katika mikutano. Mialiko ya kushiriki katika mikutano pia hufanyika kupitia mitandao ya kijamii. Ikiwa watetezi wenye ulemavu wametengwa katika mifumo ya mitandao ya kijamii, kuna uwezekano mdogo kwamba wataalikwa kushiriki katika mikutano.

Ya nne ni **upatikanaji wa rasilimali.** Hii inamaanisha kuwa na rasilimali zinazohitajika ili kushiriki kikamilifu. Hii ni pamoja na kufahamu jinsi ya kupata rasilimali na kuzisimamia, kama vile kujua jinsi ya kutuma maombi ya fedha, kuangazia matakwa ya urasimu ya wafadhili, kuweka na kudumisha miundombinu ya shirika, kukidhi mahitaji ya kisheria ya mashirika, kubuni sera na michakato ya kusimamia watu na fedha, na kadhalika. Hili limekuwa na changamoto zaidi kutokana na kuanzishwa kwa sheria, sera na taratibu za kiutawala zinazolenga kudhibiti zaidi mashirika ya kiraia (imefafanuliwa hapa chini).

## Vizuizi vya kijamii: Kutengwa na unyanyapaa

Kutojua na pia chuki kuhusu ulemavu katika jamii inaweza kusababisha watu wenye ulemavu kuaibishwa, kupuuzwa, kutengwa, au kutendewa vibaya. Katika baadhi ya matukio, imani za kitamaduni na kidini zinaweza kuongeza hatari inayowakabili watetezi wenye ulemavu kwa kiasi kikubwa.

Katika mazingira mengi, watetezi wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto za kiuchumi, kwa kuwa wametengwa kimfumo kutoka kwa taasisi za elimu na maeneo ya kazi. Hazina ya Watoto wa Umoja wa Mataifa inasema kwamba “kwa jumla, watu wenye ulemavu wana uwezekano mkubwa wa kuishi katika umaskini na uwezekano mdogo wa kupata maji safi, au kuishi katika maeneo yenye mazingira safi” (UNICEF, 2022, ukurasa. 16). Watu wenye ulemavu wako katika hatari kubwa ya kufungiwa nyumbani, hospitalini, taasisi za

magonjwa ya akili na vituo vya kizuizi. Shirika la Afya Ulimwenguni (2023) linakadiria kuwa watu wenye ulemavu hufa takribani miaka ishirini mapema kuliko wale wasio na ulemavu.

Watetezi wenye ulemavu pia wanaweza kukabiliana na hatari zaidi kwa sababu ya mazingira yao ya kisiasa. Wakati ambapo kuna migogoro, kwa mfano, watu walio na ulemavu wa kimwili wanaweza kupata ugumu zaidi kuyakimbia mashambulizi (DefendDefenders, 2022), wakati wale walio na matatizo ya kihisia, ukuaji, au kiakili wanaweza kukosa maelezo wanayohitaji ili kuelewa kinachoendelea (Shirika la Human Rights Watch, 2022).

Mitazamo ya umma na jinsi watu wenye ulemavu wanavyochukuliwa kwa jumla ni muhimu. Kama mtetezi mmoja mwenye ulemavu alivyoangazia, "Matangazo hasi ya vyombo vya habari kuhusu watetezi wa masuala ya ulemavu huathiri ufanisi wao". Matangazo ya vyombo vya habari yanayoonyesha watetezi wenye ulemavu kama watu wenye uhitaji mkubwa, dhaifu, au wenye 'kuhitaji msaada' hayasaidii. Ulemavu unaweza kuonekana kuwa hauvutii kwa umma na hivyo kutopewa kipaumbele katika vyombo vya habari.

## Ukandamizaji na kuzimwa kwa shughuli za utetezi

Ulimwenguni kote, Mataifa yamekuwa yakitumia sheria, sera, na hatua za kiutawala kuwawekea vikwazo watu katika utetezi wao wa haki za binadamu. Kwa mfano, baadhi ya mataifa yamefanya iwe vigumu kwa watu kusajili mashirika ya kiraia, na yameweka masharti ya juu kwa mashirika hayo kuripoti vitendo vyao, kuweka vikwazo vya kupokea na kuhamisha fedha, na kadhalika. Mataifa hutumia maelezo tofauti kuhalalisha haya, kwa mfano, kusema kwamba hatua hizi zinalenga kukabiliana na ugaidi, kuboresha afya ya umma, au kupunguza ufisadi na uhalifu. Hata hivyo, vikwazo hivi vimetumika dhidi ya watetezi wa haki za binadamu ili kusitisha kazi zao.

CIVICUS (2023) anasema kwamba karibu theluthi moja ya watu duniani wanaishi katika nchi ambazo **harakati za mashirika ya kiraia zimedhibitiwa**, kumaanisha, pale ambapo:

> ***Kuna kufungwa kabisa - kwa sheria na kwa vitendo - kwa harakati za kiraia. Mazingira yanayotawaliwa na hofu na vurugu, ambapo wahusika wa serikali na wasio wa kiserikali wenye ushawishi mkubwa wanaruhusiwa mara kwa mara kuwafunga, kuwajeruhi vibaya na kuua watu bila kuadhibiwa kwa kujaribu kutumia haki zao za kujumuika, kukusanyika kwa njia ya amani na kujieleza. Ukosoaji wowote wa mamlaka zinazotawala huadhibiwa vikali na hakuna uhuru wa vyombo vya habari. Intaneti imedhibitiwa sana, tovuti nyingi zimefungiwa na ukosoaji wa viongozi au utawala katika mtandao unakabiliwa na adhabu kali.***

CIVICUS anasema kwamba ni asilimia mbili tu ya watu ambao wanaishi katika nchi ambapo wanaweza kupanga, kushiriki, na kuwasiliana kwa njia huru na yenye uwazi kati yao bila vizuizi kutoka kwa serikali zao. Katika nchi nyingi duniani, CIVICUS anasema kwamba watu wanaotumia haki zao wamekuwa wakinyanyaswa, kuwekwa korokoroni, kutishwa, kuwekewa sheria zenye vikwazo, kushambuliwa, maandamano yao kuvurugwa, kukaguliwa na kuchunguzwa, kufunguliwa mashtaka na kuwekwa korokoroni.

Mbali na haya, watetezi wenye ulemavu wanaweza pia kukuta kwamba uhuru na haki zao zimewekewa vikwazo kupitia sheria, sera, na hatua ambazo zinawabagua moja kwa moja na kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Katika baadhi ya nchi, kwa mfano, wanaonekana kama watu wasio na uwezo wa kisheria wa kufanya maamuzi yao wenyewe. Baadhi ya nchi zinaweza zisiwe na sheria, sera na hatua zinazowalinda vya kutosha dhidi ya ubaguzi na kutengwa. Kwa hivyo, watetezi wenye ulemavu wanakabiliwa na ubaguzi katika viwango tofauti - katika maisha yao ya kijamii, katika

mazingirza ya utetezi wa haki za binadamu, maeneo ya kazi, na kwa sababu ya ukosefu wa ulinzi wa kisheria wa haki zao.

## Mapambano ya muda mrefu ya ushirikishwaji na haki za ulemavu

Katika mahojiano yetu, mada moja kuu iliyojitokeza ni jinsi mapambano yanavyochukua muda mrefu na pia yanakuwa magumu kufikia ushirikishwaji na hazi za ulemavu. Kama mtetezi mmoja mwenye ulemavu alivyoeleza katika mahojiano,

***Baada ya miaka na miongo kadhaa, inasikitisha kwa sababu washikadau wengine hawaelewi ulemavu na haki za ulemavu zinahusu nini. Tumekuwa tukihamasisha, tukipanga matukio na kutoa mafunzo mengi, lakini kwa njia moja au nyingine haileti mabadiliko muhimu au ya lazima. Inasikitisha kwamba tunazungumza kuhusu jambo lile lile, maswala yale yale, baada ya miaka kumi. Inatamausha, inasikitisha sana.***

Mshiriki mwingine katika utafiti huu alisema,

***Wanaharakati [wenye ulemavu] wanaweza kujifunza haraka kutoka kwa wengine na kuwa wanaharakati, lakini unawaona wakiondoka kwenye masuala ya uanaharakati, kwa sababu hawaoni matokeo chanya kutoka kwa uanaharakati wao. Kwa nini huwa tunashindwa kuwaweka wanaharakati hao kwa muda mrefu? Hiyo inaweza kuhusishwa na ukosefu wa uungwaji mkono kwa wanaharakati.***

Licha ya mapambano haya, watu wenye ulemavu wamesisitiza umuhimu wa kudumisha uhusiano, matumaini, na furaha wanapofanya utetezi ili kuleta mabadiliko.



## Kuimarisha usalama na ulinzi wa watetezi wenye ulemavu

Juhudi za kuimarisha usalama na ulinzi wa watetezi wenye ulemavu lazima zishughulikie changamoto na hatari zinazowakabili katika mazingira yao mahususi. Katika miongo michache iliyopita, Mataifa mengi, mashirika ya kiraia, na watetezi wa haki za binadamu wamekuwa wakikusanyika ili kuimarisha usalama na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu walio hatarini kupitia mipango mbalimbali ya ulinzi. Katika sehemu hii, tunaangazia mapendekezo muhimu kutoka kwa watetezi wenye ulemavu kuhusu jinsi wahusika katika sekta ya ulinzi wanaweza kuwasaidia katika usalama na ulinzi wao wakati wanapoendelea kukuza na kulinda haki za binadamu. Mapendekezo haya yamo ndani ya mfumo mpana wa mapendekezo kuhusu jinsi mifumo ya kutetea haki za binadamu inavyoweza kuwawezesha vyema watu wenye ulemavu kutetea haki zao kupitia ujumuishaji (Sehemu ya Tatu ya Mwongozo huu).

### Kuhusisha watetezi wenye ulemavu na mashirika wanayowakilisha katika kubuni na kutekeleza taratibu za ulinzi

Ili kuongeza ushirikishwaji na ufanisi wa taratibu za ulinzi, ni muhimu kuwashirikisha watetezi wenye ulemavu na mashirika yao katika kubuni na kutekeleza taratibu za ulinzi katika hatua zote. Kama mtetezi mmoja mwenye ulemavu alivyosema katika mahojiano,

> *Katika jambo lolote unalojaribu kubuni ili kuwasaidia watu wenye ulemavu... unatakiwa kuhakikisha kwamba wao wenyewe wanahusika katika kile unachotaka kuwafanyia... haitakuwa vyema kubuni suluhu pale ambapo hawajahusika, kwa sababu mara nyingi, unaweza kupata kwamba mambo fulani hayakuzingatiwa. Na kumbuka kwamba, hadi kufikia wakati wa kuzindua suluhisho hiyo, tayari umetumia rasilimali zako. Kwa hivyo, rasilimali hizo huwa zinapotea pale ambapo njia sahihi na stahiki haikufuatwa. Ukitaka kubuni jambo lolote... wahusishe watu wenye ulemavu kuanzia mwanzo – kuanzia kuandika malengo hadi ufuatiliaji na kutathmini ubora wa jambo hilo... Kwa kufanya hivyo, naamini jambo lako litafaulu, tuseme kwa asilimia 80%. Na pia litakubalika na watu wenye aina tofauti za ulemavu.*

Kwa kuzingatia hususan suala la mafunzo, mlinzi mwingine mwenye ulemavu alipendekeza,

> *... kuhusisha watetezi wenye ulemavu na wasaidizi wao au walezi katika kupanga mbinu bora za kuhakikisha ushiriki wao na kujifunza wakati wa utoaji mafunzo. Kwa mfano, katika mafunzo ya usalama wa kidijitali, baadhi ya maneno ya kiufundi yanaweza kukosa kueleweka kwa urahisi na watafsiri wa lugha ya ishara, au baadhi ya maonyesho ya vitendo yanaweza kuwatenga washiriki wenye ulemavu wa kutoona. Hili linatakiwa kuangaliwa kabla ya kutekeleza shughuli hizo.*

Ili kumsaidia mtetezi mwenye ulemavu katika utetezi wake, ni muhimu kumsikiliza, kumuuliza ni nini anataka kufanya, anataka kutimiza nini, na vikwazo vinavyomkabili katika kutekeleza hayo. Kila mtetezi ana hisia na matukio ya kipekee kuhusu ulemavu, na anafaa kuongoza hatua ya kutafuta suluhu na majibu kwa hali yake mwenyewe.

Mifano mizuri ni kama:

- **Katika makongamano, mikutano, na warsha,** kuweka ajenda zinazoongozwa na watetezi wenye ulemavu. Wafunze wasimamizi na waratibu wa mikutano kuhusu masuala yanayowahusu watu wenye ulemavu na njia za kutimiza mahitaji yao. Pangia muda wa mapumziko wa hisia katika programu

na pia epuka ajenda ya mazungumzo iliyoharakishwa na pia yenye taarifa nyingi sana ndani yake. Buni shughuli ambazo zinajumuisha watu walio na aina tofauti ya miili - usifikirie kwamba wanapaswa kwenda au kukaa kwa njia fulani. Toa njia mbadala, kwa mfano, kuwepo na mazoezi tofauti ya kimwili. Tenga fedha ili mtetezi apate msaidizi anayeelewa mahitaji yake, na hivyo kupunguza utegemezi kwa watu wanaomzunguka. Toa ufadhili wa ushiriki wao katika hafla, kwa mfano, wanaposhiriki kama wasemaji, badala ya kutarajia waifanye kama watu wa kujitolea wasiolipwa, kwa kutambua kwamba watu wenye ulemavu mara nyingi wanakabiliwa na ukosefu wa ajira. Tambua mapema mahitaji ya ufikikaji kwa kila mshiriki na upange kuwatimizia mahitaji kwa njia inayofaa. Panga matukio kama haya vizuri, ukiwa na rasilimali za kutosha, na uwasilishe habari za utaratibu wake mapema.

- Wakati wa **kutoa tena misaada** au **kutoa misaada ya dharura**, hakikisha kwamba ujumuishaji wa masuala ya ulemavu ni kigezo au mojawapo ya masharti katika jinsi watu wanavyotuma maombi ya kupata ufadhili. Weka wazi kuwa watetezi wenye ulemavu ni kundi lengwa na muhimu katika msaada huo. Zingatia jinsi hatua ya kufanya maamuzi kuhusu uharaka na uhalali wa misaada hiyo inavyokandamiza, kwa mfano, kwa kuwapa kipaumbele wanaharakati wanaotetea haki za kiraia na kisiasa kwa kupitia njia ambazo ni wazi, na vitendo vyenye hatari zaidi. Hakikisha kwamba mchakato wa kuomba msaada wa ufadhili unapatikana kwa njia sawa na watu wote, ni rahisi kuelewa, na rahisi kujaza, ikiwemo kupitia fomu ya maombi ya ufadhili na tovuti ambayo taarifa zinachapishwa. Jumuisha sehemu katika fomu ya maombi ambapo watetezi wenye ulemavu wanaweza kueleza jinsi mahitaji yao mahususi yanaweza kushughulikiwa na pia tenga bajeti kwa ajili ya kukidhi mahitaji yanayohitajika.

- Kuunda na kutengeneza **ufadhili wa elimu** ambao unaangazia jinsi watetezi wenye ulemavu wanaelewa na kukabili masuala ya usalama, ulinzi, hatari na uzima, na pia **ufadhili wa vitendo vya furaha** ambao unawapa nafasi watu wenye ulemavu kushiriki katika mambo yanayowapa furaha, kushabikia uthabiti, na kuunga mkono afya na uzima (kama zile zinazotolewa na hazina ya the Borealis Philanthropy Disability Inclusion Fund).

- Katika **mipango ya muda ya kuhama**, zingatia mahitaji mahususi ya watu wenye ulemavu, kama vile makazi na ofisi zinazoweza kufikiwa kwa urahisi, utoaji wa matibabu, usafiri unaofaa, na usaidizi katika mahitaji ya kibinafsi.

- **Kutoa fursa za mafunzo na kujenga uwezo** wa watetezi wenye ulemavu kuhusu mada kama vile: kuelewa dhana na mawazo yenye mapendeleo (kwa mfano, kuhusu jinsia, utambulisho kuhusu mahusiano ya kimapenzi na jinsia tofauti, uhuru wa kidini); kufanya tathmini za hatari na juhudi za kuzipunguza, kutengeneza mipango ya kujilinda; kupata rasilimali za uanaharakati, ikijumuisha ufadhili, watu wa kujitolea, na mitandao ya kijamii; kupata rasilimali za kuimarisha ulinzi na mipango iliyoundwa mahsusi kwa watetezi wa haki za binadamu walio hatarini; maendeleo ya mashirika; na kuangalia ustawi wa mtu binafsi na wa jamii kwa jumla.

Sanduku 3

## Kanuni saba zinazoimarisha kanuni nzuri za ulinzi

(Aliyekuwa wakati huo) Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu hali ya watetezi wa haki za binadamu, Michel Forst, katika ripoti yake kwa Baraza la Haki za Kibinadamu mwaka 2016 (Forst, 2016), alieleza kanuni saba zifuatazo ambazo zinaimarisha kanuni nzuri za ulinzi.

**Kanuni ya 1:** Wanafaa kufuata mfumo wa kuzingatia haki katika kuangalia masuala ya ulinzi, kuwawezesha watetezi kujua na kudai haki zao na kuongeza uwezo na uwajibikaji wa wale walio madarakani katika kuheshimu, kulinda na kutimiza haki.

**Kanuni ya 2:** Wanafaa kutambua kwamba watetezi ni wa aina tofauti; wanatokea katika mazingira tofauti, malezi, tamaduni, na mifumo tofauti ya imani. Tangu zamani, huenda wakakosa kujitambulisha au kutambuliwa na wengine kama watetezi.

**Kanuni ya 3:** Wanapaswa kutambua umuhimu wa jinsia katika kuwalinda watetezi na kutumia mbinu ya mkingamano katika kutathmini hatari na kubuni mipango ya ulinzi. Pia wanapaswa kutambua kwamba baadhi ya watetezi wako katika hatari zaidi kuliko wengine kwa sababu ya utambulisho wao na kile ambacho wanafanya.

**Kanuni ya 4:** Wanapaswa kuzingatia "usalama kamili na wa jumla" wa watetezi, yaani usalama wao wa mwili, usalama wa kidijitali na ustawi wao wa kisaikolojia na kijamii.

**Kanuni ya 5:** Wanafaa kukiri kwamba watetezi wana mtandao unaowaunganisha. Hawapaswi kuzingatia haki na usalama wa watetezi binafsi pekee, bali pia wajumuishe vikundi, mashirika, jamii na wanafamilia ambao pia huathiriwa na hatari zinazowakabili.

**Kanuni ya 6:** Wanapaswa kuwahusisha watetezi katika uundaji, maamuzi, utekelezaji na katika kutathmini mikakati na mbinu za kuwalinda. Kuwahusisha watetezi ni jambo muhimu katika usalama wao.

**Kanuni ya 7:** Wanapaswa kuruhusu mabadiliko kufanywa katika mipango yao ili kuhakikisha inalingana na mahitaji na hali maalum ya watetezi.

## Kukadiria hatari kwa mbinu tofauti

Watu wenye ulemavu ni tofauti, na makabiliano yao binafsi ya ulemavu na hatari yanaweza kuwa tofauti sana. Kama ilivyoelezwa hapo juu, watetezi wenye ulemavu wanakabiliwa na hatari ambazo watetezi wasio na ulemavu hawakabiliani nazo. Mazingira yanayoweza kuwa salama kwa mtu asiye na ulemavu yanaweza kuwa hatari kwa mtu mwenye ulemavu. Ni muhimu kwa juhudi za kutathmini hatari na mbinu za kuwalinda kutambua kwamba makabiliano ya mtu binafsi ya hali hatari yanaweza kuongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na ulemavu wake.

Kwa mfano, mwanamke mtetezi wa haki za binadamu mwenye ulemavu wa kimwili anaweza kuomba msaada wa kusafiri kwa teksi, kwa sababu hii ndio njia pekee ambayo ni salama kwake kutumia katika eneo lake. Mwingine anaweza kuomba msaada wa kifedha ili kulipia gharama za msaidizi wake katika kuhudhuria mkutano wa utetezi. Wale wanaotathmini maombi hayo wanaweza kuuliza ni kwa nini usaidizi kama huo ni muhimu na unahusiana vipi na harakati za 'utetezi', bila kutambua umuhimu wa masuala ya ufikikaji na umuhimu wa uanaharakati ambao sio wa moja kwa moja.

Mbinu ya mkingamano ya kukadiria na kudhibiti hatari ni muhimu katika kufichua kiini cha hatari na uwezo wa kuzipunguza. Wahusika katika sekta ya ulinzi wanaweza kufanya kazi na watetezi wenye ulemavu na mashirika yao ili kukagua itifaki wanazotumia kukadiria hatari na kufanya maamuzi kuhusu msaada wa ulinzi unaotolewa kwa watetezi wenye ulemavu.

## Kutetea sheria, sera na taratibu za kuwawezesha watu wenye ulemavu kutumia haki yao ya kutetea haki za binadamu

Kwa sababu watetezi wenye ulemavu wanaathiriwa na sheria, sera na taratibu zinazolenga kukandamiza kazi ya haki za binadamu na kupunguza nguvu ya shughuli za utetezi, moja kwa moja na kwa njia zisizo za moja kwa moja, wahusika katika sekta ya ulinzi wanahitaji kuzingatia kuandika na kuhifadhi hati, kuchambua na kukabiliana na athari hizi. Katika baadhi ya matukio, mabadiliko yanahitajika; katika matukio mengine, sheria na sera mpya zinahitajika ili kulinda haki za watu wenye ulemavu. Ni muhimu kuhakikisha kuwa serikali zinawajibika katika kutekeleza majukumu yao chini ya sheria ya kimataifa ya haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na mkataba wa CRPD.

## Kuwezesha ujenzi wa mitandao na mifumo ya uanaharakati miongoni mwa watetezi wenye ulemavu

Washiriki katika utafiti huu waliangazia umuhimu wa kujenga mshikamano na watu wanaosimamia masuala tofauti. Kama ilivyoangaziwa katika Sehemu ya 2.2, watu wengi wenye ulemavu wanaokuza na kulinda haki hawajioni kama ni watetezi wa haki za binadamu. Wengi pia hawajui kuhusu mfumo wa ulinzi wa kimataifa kwa watetezi wa haki za binadamu walio katika hatari. Kuwaunganisha na wahusika katika sekta ya ulinzi pamoja na rasilimali katika mazingira yao kunaweza kuimarisha kazi zao na kuwasaidia kuhimili na kukabiliana na upinzani.

Vile vile, hatua nyingine muhimu ni kuhakikisha kuwa vikundi vya haki za walemavu vinaunganishwa na mitandao na miungano ya haki za binadamu ya ndani ya nchi, ya kikanda, na kimataifa. Hii inaweza kusaidia kuongeza ufahamu kuhusu masuala ya haki za ulemavu na kuhakikisha kwamba mitazamo ya kipekee




ya watu wenye ulemavu inawakilishwa ndani ya mifumo ya utetezi wa haki za binadamu.

Kuhusu haki za ulemavu haswa, washiriki katika utafiti huu walipendekeza **mbinu ya ulemavu inayojumuisha watu wenye ulemavu wa aina yoyote**, uwe wa kimwili, kitabia, au kihisia, au ukuaji. Kama mtetezi mmoja wa haki za walemavu alivyosema,

> ***Mshikamano** unaweza kufasiriwa kama kujumuisha aina tofauti za watu. Tunahimiza mashirika tofauti ya masuala ya ulemavu kufanya kazi pamoja... sauti yenye umoja daima huwa na nguvu kuliko sauti moja ya mtu binafsi. Mshikamano katika muktadha huo unamaanisha kuwa hatuachi kikundi chochote cha walemavu nyuma... hatuzingatii tu mahitaji yetu maalum, lakini tunaelewa kuwa kuna mahitaji tofauti... Aina hiyo ya 'kufanya kazi pamoja' inaweza kusaidia harakati za haki za walemavu na kufanya sekta ya ulemavu kuonekana zaidi. Kisha kukuza haki zao inaweza kuwa rahisi - ni hatua ya pamoja, na tunaweza kutarajia matokeo yanayoonekana zaidi.*

Hata hivyo, pia walitambua kuwa baadhi ya watetezi walitaka tu kuzingatia ulemavu wao wenyewe badala ya kujihusisha na harakati pana za ulemavu.

Katika baadhi ya visa, watu wenye aina fulani za ulemavu wanaweza kutofahamu aina nyingine za ulemavu. Alipoulizwa kulinganisha makabiliano yake binafsi katika kutetea watu wenye ulemavu wa akili na ukuaji ikilinganishwa na ulemavu wa aina nyingine, mtetezi mmoja wa haki za ulemavu alisema katika mahojiano,

> ***Ni tofauti sana. Ni tofauti sana. Ni tofauti sana.***
> ***Nadhani hata katika mazingira ya ulemavu, kuna wale ambao wametengwa zaidi...***

> *[wanafikiria"] "sawa, wale walio na ulemavu wa akili, hatuwezi kuwashirikisha". Hata ndani ya [harakati za ulemavu] kuna mambo yanayofanywa tu kuonyesha kwamba aina nyinginezo za ulemavu zimezingatiwa, kama ishara ya usawa..*

Washiriki katika utafiti huu pia walitahadharisha kuhusu ukosefu wa usawa katika uongozi na uwakilishi katika harakati za walemavu. Kama mtetezi mmoja wa haki za ulemavu alivyosema katika mahojiano,

> *Nimeona watu ambao kwa hakika wametoka mahali ambapo wamehisi wamekandamizwa, na wameingia uongozini, na wamesahau walikotoka. Na hilo linaweza kutokea katika mazingira yoyote ... mamlaka ni suala kubwa sana kwa sababu ya ukandamizaji ambao umefanywa kuwa kawaida katika jamii ... bila shaka, kuna wakati ambapo ulemavu wa wanaharakati unaweza kuwachochea kuwa na shaka kuhusu kudumu kwao uongozini ... na [wanataka] kudumisha mamlaka hayo mara tu wanayoyapata.*

Kanuni za mfumo unaopendelea wanaume zaidi katika jamii pia zipo katika harakati za haki za binadamu, na hii inaweza kusababisha tabia ya kudhalilisha, na unyanyasaji wa kijinsia. Ni muhimu kutambua hali ya kutofautiana baina ya watu ndani ya mifumo ya ulemavu na kuchunguza uhusiano kati ya wenye mamlaka na wasiokuwa nayo kwa darubini inayozingatia vigezo kadhaa. Hii inaweza kusaidia kufichua ukosefu wa usawa katika nafasi, sauti, na uwakilishi miongoni mwa vikundi na jamii, na kusaidia kutambua ni sauti za nani zinazopuuzwa au kunyamazishwa.

## Kukuza 'ustawi katika vitendo' kati ya watetezi wenye ulemavu

Kumekuwa na uzingatiaji mkubwa miongoni mwa watetezi wa haki za binadamu kuhusu umuhimu wa afya nzuri na ustawi katika harakati za haki za binadamu lakini pia kuhusu changamoto katika kushughulikia mada hii. Tamaduni za taratibu za haki za binadamu zinathamini ushujaa, kujitolea, na kutokuwa na ubinafsi, na hivyo kusababisha watetezi wa haki za binadamu kuhisi kana kwamba wanakosea wanapozingatia kujitunza (Barry na Đorđević, 2007; Barry na Nainar, 2008; Nah, 2021). Majadiliano kuhusu afya ya kiakili na ya kihisia yana mizizi katika dhana za kitamaduni, kisiasa, na mambo ambayo ni mwiko kijamii; watetezi wa haki za binadamu wana wasiwasi kuhusu kuonekana kuwa wagonjwa au hawawezi kustahimili. Mshiriki mmoja katika utafiti huu alisema, "tunachukulia kimakosa kuwa afya ya akili ndiyo gharama tunayopaswa kulipa kwa ajili ya [harakati zetu]".

Katika utafiti huu, watetezi wenye ulemavu walitueleza kwamba afya na uzima wao ulihusishwa na ukosefu wa usalama wa kifedha; hisia ya 'kuishi chini ya uwezo wako'; kuonekana kama umekosa thamani katika jamii; na hofu ya kukataliwa, kukabiliwa na unyanyapaa, na kutengwa. Kama mtetezi mmoja mwenye ulemavu alivyosema katika mahojiano, "kukubaliwa, kuonekana, ni muhimu kwa afya na uzima". Pia walisisitiza changamoto walizokuwa nazo katika kudumisha ustawi wa kimwili. Mtetezi mmoja mwenye ulemavu alisema, "tunakumbana na vikwazo zaidi linapokuja katika suala la fursa na huduma za kufanya mazoezi [ya kimwili]". Kuishi tu maisha ya kila siku kunaweza kuwa changamoto. Akielezea uhusiano wake wa kila siku kuhusu uzima, mtetezi mwanamke mwenye ulemavu alisema katika mahojiano,

> *Kwa kweli ni mkusanyiko wa vitu vidogo sana... ambavyo hujilimbikiza kadri siku yako inapokwenda... hatimaye, unafika mwisho*

*wa siku, na...umechoka tu na kuishiwa na nguvu kabisa. Kwa sababu ya mambo madogo ambayo - ikiwa yangerekebishwa tu - ungejihisi vizuri zaidi ... kila moja ya mambo hayo yanaonekana kuwa madogo kivyake, lakini unapoyaunganisha yote pamoja ... ni mengi sana. Ni shida tupu. Inachosha.*

*Kwa hivyo... ili niwe na afya njema ya akili, ninahitaji kuondosha vitu hivi vidogo ambavyo ni kero ya mara kwa mara katika maisha yangu... ni kero la kila wakati, sio kwa sababu ndivyo hali ilivyo, ni kwa sababu watu hawafikirii kuhusu watu kama mimi wakati wanatengeneza vitu... [na unapoenda] kuwaambia kuvihusu, hawawezi kuvibadilisha tena kwa sababu hatua hiyo ni ya 'gharama kubwa' au wanaona kuwa ni 'kazi nyingi'*

Na, kama mtetezi mwingine mwenye ulemavu alivyobainisha, "watu wenye aina fulani ya ulemavu hawawezi kuishi bila kufikiria kuhusu afya na uzima wao". Tuligundua katika utafiti huu kwamba watetezi wenye ulemavu walikuwa wakikabiliana na jinsi ya kukwepa vikwazo vinavyowazuia kufanya mambo kila mara. Walifurahia mazungumzo kuhusu ustawi wao, ambao mara nyingi haukuzingatiwa. Walisisitiza kuhusu umuhimu wa mitazamo chanya ya mazungumzo kuhusu ustawi wao - kama vile kutoa kipaumbele kwa dhana za uhimilivu, furaha, uwezeshaji na nguvu.

Walieleza kwamba kuwepo katika vikundi vya kuwasaidia watu wa tabaka moja, kuungana na watu wenye nia moja katika maeneo salama, mambo ya kibinafsi yenye kuleta furaha (kama vile kutengeneza bustani na kushiriki katika kuunda sanaa), kushiriki katika taratibu za imani fulani, likizo na mapumziko ya kuimarisha afya na uzima wa kimwili, na vipindi vya matibabu ya kisaikolojia, viliimarisha ustawi wao. Wale waliofanyia kazi kesi ngumu za haki za binadamu pia walisema kuwa inasaidia sana pale kunapokuwa na fursa za kuelezea wengine kuhusu kazi zao, na kuomba ushauri kuhusu jinsi ya kushughulikia kesi fulani na hali ngumu zinazowakabili. Kulikuwa na mapendekezo makubwa ya kufanya utafiti zaidi na kutafakari kuhusu ustawi wa watetezi wenye ulemavu katika harakati za haki za binadamu.

# 3 Kuimarisha ujumuishaji katika harakati za kutetea haki za binadamu

Ujumuishaji unamaanisha kuheshimu haki kamili za binadamu wote, kutambua utofauti, na kuhakikisha kwamba kila mtu anaweza kushiriki kikamilifu katika michakato na shughuli za haki za binadamu, bila kubaguliwa kwasababu ya umri, jinsia, ulemavu, hali ya afya, kabila, au vigezo vingine vyovyote. Ujumuishaji sio tu kuhusu kuhusisha au kuunganisha watu wenye ulemavu katika shughuli tofauti, pia unahusu kuzingatia haki kwa kutambua vikwazo vinavyozuia ushirikishwaji na kuchukua hatua za kukabiliana nazo. Katika sehemu hii, tunaangazia mapendekezo kutoka kwa washiriki katika utafiti huu kuhusu jinsi harakati za kutetea haki za binadamu zinaweza kuwawezesha watu wenye ulemavu ili kutetea haki zao kwa ufanisi zaidi.

## Kuzingatia ushiriki wenye maana na uongozi wa watu wenye ulemavu

**'Hakuna kuamua chochote kinachotuhusu bila kutuhusisha'** imekuwa kauli mbiu na ujumbe muhimu kutoka kwa vuguvugu la haki za walemavu kwa miongo kadhaa. Hii ina maana kwamba watu wenye ulemavu lazima washiriki katika maamuzi yanayowahusu; hakuna kinachowahusu kinapaswa kupangwa au kutekelezwa bila michango yao. Kuhusisha watu wenye ulemavu katika michakato ya kufanya maamuzi husababisha kuzingatiwa kwa kina zaidi kwa mahitaji yao. Watu wasio na ulemavu wanaweza kukosa kuelewa tofauti, changamoto na mambo fulani kuhusu ujumuishaji wakati wa kubuni shughuli mbalimbali. Kama mtetezi mmoja mwenye ulemavu alivyosema,

> ***Watu wenye ulemavu mara nyingi huwa na maarifa ya kipekee kuhusu ulemavu wao na hali zao. Wana uwezo wa kuchangia kikamilifu na kwa njia ya maana ili kuunda maeneo jumuishi ya kazi pamoja na miradi katika hatua zote. Kwa hivyo, mashirika ya watu wenye ulemavu yanapaswa kushauriwa kama wataalam katika kutambua na kukabiliana na vikwazo vinavyowakabiliwa na watu wenye ulemavu.***

Mtetezi mwingine mwenye ulemavu alisisitiza, "Ni muhimu vile vile kuwa makini na kuchagua watu wenye ulemavu wanaowakilisha aina tofauti za ulemavu na wanaotokea katika mazingira tofauti". Ushiriki wa watetezi wenye ulemavu lazima upangiliwe tangu mwanzo wa tukio, kwa sababu inachukua muda kupata washiriki, kuunda mipango shirikishi ambayo ni ya maana, na kupanga jinsi ya kukidhi mahitaji yao tofauti kwa njia inayofaa. Ni muhimu kuwaalika na kuwajumuisha watetezi wenye ulemavu katika masuala yote ya haki za binadamu, sio tu wakati ambapo ulemavu ndio uko kwenye ajenda.

### Kuajiri watu wenye ulemavu na kukidhi mahitaji yao kwa njia inayoridhisha

**Kuajiri watu wenye ulemavu** ni hatua muhimu katika kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanashiriki na kuleta manufaa katika harakati za kutetea haki za binadamu. Tafiti kadhaa zinaonyesha kuwa mashirika ambayo huchukulia kwa umakini suala la kukidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu hunufaika pakubwa kutokana na utendaji thabiti wa shirika – huwa inaongeza sifa za eneo hilo la kazi, na inavutia watu wengi wenye vipaji (Accenture, 2018). Mashirika ya haki za binadamu yanapaswa kuongoza mipango kama hii na kuwa mifano ya kuigwa na wengine.

Jibu ambalo mashirika mengi hutoa ni kwamba watu wenye ulemavu hawatumi maombi ya kazi zinazotangazwa. Ili kukabiliana na hili, makampuni yanaweza kushirikiana na mashirika ya watu wenye ulemavu ili kutambua kwa pamoja watu wenye ulemavu waliohitimu kwa nafasi za kazi na kutoa mafunzo kuhusu ulemavu kwa wafanyakazi wanaohusika katika kuajiri watu. Mashirika yanaweza kuweka malengo ya kuajiri na kuwatunza watu wenye ulemavu na kufuatilia maendeleo yao wenyewe katika kufikia malengo haya. Kwa mfano, kuna mashirika ambayo yanawahimiza watu wenye ulemavu kuomba kazi na ambayo yanahakikisha usaili kwa waombaji wenye ulemavu ambao wanakidhi vigezo vya chini vya nafasi za kazi.

Suala lingine la kupewa kipaumbele ni kwa mashirika ya haki za binadamu kukidhi mahitaji muhimu kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi. Baadhi ya mameneja wanahofia kuwa kuajiri watu wenye ulemavu kutaongeza gharama ambazo mashirika yao hayawezi kukimu. Hata hivyo, kama vile mtetezi mmoja mwenye ulemavu alivyoeleza,

> *Wakati mashirika yanapofikiria kuwa "tukiwajumuisha watu wenye ulemavu kwenye shirika letu itavuruga bajeti yetu", hili husababisha kutengwa... Mara nyingi, dhana hii haihusiani na ukosefu wa bajeti bali nia ya kufikiria kuhusu hatua gani zinaweza kuchukuliwa ili kushughulikia masuala haya ipasavyo. Inaweza kuwa rahisi na nafuu*

Mtetezi mmoja mwanamke mwenye ulemavu alisisitiza umuhimu wa kuwa na uwezo wa kubadilisha maoni na maamuzi ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu, akisema,

> *kubadilika kwa mipangilio ya kazi, kama uwezekano wa kufanyia kazi nyumbani, ni muhimu kwa watu wenye ulemavu. Iwapo ni lazima nifanyie kazi ofisini, basi kuwa na fursa ya kuondoka kazini mapema, kabla ya msongamano wa magari barabarani kuanza, kunaweza kuboresha hali yangu kwa kuwa nina changamoto zinazohusiana na usafiri. Kwa mfano, katika [mji wangu], mabasi ya umma huwa na haraka kila wakati, kwa hivyo, wakiniona nimekalia kiti cha magurudumu wakati watu ni wengi, wanaharakisha kuondoka na hawanichukui, kwasababu wanafikiria nitawapunguzia kasi ya kazi.*

Utoaji wa huduma muhimu ili kukidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu ni muhimu - hii haipaswi kuonekana kama fadhila au kesi maalum, lakini inafaa kuonekana kama njia ya kuwawezesha kupata haki zao. Kuweka mipango ya kukidhi mahitaji yao kwa njia ya kuridhisha ni muhimu na inapaswa kujumuishwa katika bajeti za kila mwaka.

## Kushirikiana na watetezi wenye ulemavu na mashirika wanayowakilisha

Ubia ni mojawapo ya njia za kuwashirikisha watetezi wenye ulemavu kwa njia ya maana. Hii inaweza kuwa njia ya kujifunza kwa pande zote katika ushirika huu. Kama mtu mmoja aliyeshiriki katika utafiti huu alivyohimiza,

> *... Ushirikiano, ushirikiano, ushirikiano, kwasababu hii ndio njia mwafaka ya kupata maarifa tofauti. Hivi ndivyo utakavyoelewa utofauti wa watu na kuwajumuisha. Hivi ndivyo unavyojua lugha sahihi ya kutumia. Hii itasaidia shirika kukua na kujua kwa kina kila haki ya binadamu wanayohitaji kuzingatia.*

Ubia unaweza kufungua fursa kwa mashirika madogo, kuyasaidia kukuza mifumo yao, michakato, mitandao na jinsi yanavyochukuliwa au kuonekana na umma. Kama mshiriki mmoja alivyoangazia, "Lengo la mashirika ya watu wenye ulemavu ni kuonekana, kujulikana, kutoa kauli kuhusu mada zinazotuhusu. Kwa njia hii, unaweza pia kubadilika kutoka kuwa shirika ambalo halikuwa linapata ufadhili wa moja kwa moja na kuanza kuupata moja kwa moja".




## Kusaidia kuimarisha uongozi wa watetezi wenye ulemavu

Kumekuwa na mapendekezo mengi katika utetezi wa watu wenye ulemavu kuongoza mambo yao wenyewe. Akitoa maoni yake kuhusu uwiano kati ya majukumu na mahusiano kati ya watu wenye ulemavu na washirika wanaofanya kazi kwa mshikamano nao, mtetezi mmoja mwenye ulemavu alieleza katika mahojiano,

> ***Harakati za kutetea haki za walemavu kihistoria zimekumbana na ukosefu wa uhuru katika suala lolote, hasa kuhusu utetezi. Bado tunahitaji kupigana vikali ili kutambuliwa kuwa mtu mwenye haki ya kuzungumza. Ni muhimu kwenu nyinyi [waungaji mkono wasio na ulemavu] kufahamu jukumu lenu ni nini - kuunga mkono na sio kuongoza. Ikiwa hilo haliko wazi kwako, unachangia katika kuwepo kwa tatizo lililopo.***
>
> ***Pili, ajenda ya utetezi inafaa kutathminiwa na watu wenye ulemavu. Ninyi [waungaji mkono wasio na ulemavu] hamna haki ya kuamua ajenda. Unaweza kusaidia lakini tambua kuwa wewe sio sehemu ya mfumo wa ulemavu.***
>
> ***Mwisho, mchango chanya zaidi, kuna maeneo fulani ambapo watu wenye ulemavu hawawezi kufikia kwa sababu hatuna uwezo, ujuzi, na hatutambuliwi kama watu ambao wanaweza kuwa washirika. Jukumu la marafiki ni kufungua milango hiyo, ya vyuo vikuu vyao, vituo vya utafiti, kwa sababu wana nafasi nzuri kuliko sisi. Tunatarajia hilo.***

Ni muhimu kuzingatia uwiano wa nani mwenye mamlaka zaidi katika mipango ya ubia, na kuhakikisha kuwa ushirikiano ni wa heshima na wa kuwawezesha watu wenye ulemavu kuwa na nguvu zaidi.

# Kukiri na kukabiliana na ukandamizaji uliofanywa kuwa kawaida

Ni muhimu kutambua na kukabiliana na mfumo wa ukandamizaji uliofanywa kuwa kawaida wa kutathmini uwezo na thamani ya watu kulingana na vigezo fulani ndani ya mifumo ya utetezi wa haki za binadamu. Sisi sote tunafaa kuzingatia mitazamo yetu wenyewe, upendeleo, na mawazo tunayodhania ni ya kawaida kuhusu ulemavu. Pia tunahitajika kutambua na kukabiliana na ubaguzi wa kijinsia, chuki dhidi ya wanawake, ubaguzi wa rangi, chuki dhidi ya raia wa kigeni, na aina

nyingine yoyote ya ubaguzi ambayo inapokonya watu haki na hadhi yao. Kizuizi kikubwa cha kuanzishwa kwa huduma jumuishi ni kimya kuhusu suala hili miongoni mwa watu wasio na ulemavu.

Ingawa mashirika mengi ya haki za binadamu yanakubaliana kimsingi katika umuhimu wa kufanya sehemu zao za kazi na shughuli zao kuwa jumuishi, wakati mwingi hilo halifanyiki. Katika utafiti huu, watetezi wenye ulemavu waliangazia kuenea kwa hatua zilizochukuliwa kwa nia tu ya kuonyesha au kutoa ishara kwamba watu wenye ulemavu wamezingatiwa. Mtetezi mmoja mwenye ulemavu aliyejaribu kuhimiza shirika lake la kutetea haki za binadamu kujitolea kuhakikisha kuwa ni jumuishi kwa ulemavu alielezea kazi hiyo kama "safari ya upweke".

## Kuendelea kujifunza kuhusu ulemavu na haki

Vikwazo katika jamii vinavyosababisha ulemavu mara nyingi havitambuliwi na havionekani. Ufahamu na maelezo kuhusu haki za ulemavu na haki kwa ujumla yanaweza kubadilika kwa haraka. Kama mshiriki mmoja katika utafiti huu alivyosema, "uelewa wa masuala ya ulemavu na athari zake ni hatua muhimu ya kwanza kwa mashirika kuwa jumuishi zaidi". Mwingine alisisitiza haja ya "kufahamu utofauti wa ulemavu na mahitaji tofauti ya makundi mbalimbali". Kufikia kiwango kinachohitajika cha ujumuishi kunahusisha mtu kukiri kuwepo na mapendeleo ya kibinafsi, kuwa tayari kufanya makosa na kuomba msamaha, na daima kudumisha mtazamo wa kujifunza kila wakati.

Mashirika yanaweza kuwezesha mafunzo haya kwa njia tofauti, kwa mfano kwa kuhakikisha kuwa programu za kuwakaribisha wafanyikazi wapya zinashughulikia mada zinazohusiana na ulemavu na ujumuishaji; kuwaalika watetezi wenye ulemavu kutoa mafunzo na ujuzi wao mara kwa mara; na kuandaa mikutano au mafunzo ya pamoja kati ya washirika, wafadhili, na washikadau wengine.

Watu wengi hawatangamani sana na watu wenye ulemavu, na hivyo wanaweza kushangazwa au kuchanganyikiwa wakati watu wenye ulemavu wanaonyesha tabia ambazo hazijazoeleka au zisizotarajiwa. Katika mojawapo ya mahojiano yetu, mtetezi wa watu wenye ulemavu wa akili na ukuaji alieleza jinsi alivyomleta mtoto mwenye usonji kwenye ukumbi wakati wa programu ya mafunzo ya ujumuishaji wa ulemavu kwa wataalamu wa afya. Aliwaona wataalamu hao wakiwa "katika hali ya mshtuko" walipomuona mtoto akinung'unika, akionyesha kuumia, na akitembea-tembea, kwa kuwa hawakuwa wamezoea tabia hizi. Alisema, "Kile ambacho hujakiona, huwezi kukielewa au kushirikiana nacho". Mafunzo huhusisha kuingiliana na watu walio na aina tofauti za ulemavu na kutafakari dhana na matarajio yetu kuhusu tabia, mawasiliano na mwingiliano wa kijamii.

Kujifunza pia humaanisha kuheshimu haki ya watu wenye ulemavu kutoshiriki katika mazungumzo kuhusu ulemavu. Kama mtetezi mwanamke mwenye ulemavu alivyosema,

> ***"Watu wengi wenye ulemavu wamekabiliwa na maswali yanayohusisha mambo ya kibinfasi na ya kudhalilisha, kwa hivyo ingawa lengo la mazungumzo haya ni kuondoa dhana potovu kuhusu ulemavu, watu tofauti watakuwa na mipaka tofauti kuhusu mambo ambayo wako tayari kuzungumzia".***

## Kujumuisha ulemavu katika jamii

Njia moja ya kukabiliana na ukandamizaji uliofanywa kuwa kawaida ni **kujumuisha ulemavu katika jamii**, yaani, mchakato wa kujumuisha mitazamo ya ulemavu na mahitaji ya watu wenye ulemavu katika sera zote, programu, na shughuli zote za shirika. Hii inaweza kuhusisha:

- Kubuni **mkakati wa kujumuisha ulemavu** ambao unakubaliwa na kuthaminiwa na uongozi wa shirika, kuhakikisha unapewa kipaumbele na kutekelezwa katika maeneo yote ya shirika.
- Kufanya **tathmini ya mahitaji ya ulemavu** kupitia kwa watetezi wenye ulemavu na mashirika yao ili kutambua vikwazo vya ujumuishaji na upatikanaji wa huduma na vifaa muhimu ndani ya shirika na miradi yake.
- Kuanzisha **kikundi au jopo maalum la ushirikishwaji wa ulemavu** linajumuisha wafanyakazi wanaowakilisha idara mbalimbali na wadau muhimu wa ulemavu ili kuongoza juhudi za kuunda na kutekeleza sera na harakati zinazojumuisha ulemavu.
- **Kubuni na kutekeleza sera na desturi zinazojumuisha ulemavu**, kama vile zile zinazoimarisha upatikanaji wa huduma na vifaa muhimu, muundo wa vifaa na huduma, na kukidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu.
- Kutoa **mafunzo ya kuimarisha ufahamu wa ulemavu** kwa wafanyakazi wote, ikiwa ni pamoja na kuelewa ulemavu ni nini, upatikanaji wa huduma na vifaa muhimu, na ushirikishwaji, na maelezo ya mara kwa mara kuhusu masuala hayo.
- Kuanzisha **mfumo wa kutathmini na kufuatilia utekelezaji** kwa kuzingatia viashirio na vigezo wazi, pamoja na vifaa, ili kutathmini hatua zilizopigwa katika kutimiza malengo ya ujumuishaji wa ulemavu na kutambua ni maeneo gani yanayohitaji kufanyiwa marekebisho.
- Kuteua **mtu maalum anayesimamia masuala ya usawa wa ulemavu** ili kusaidia na kuongoza michakato yote iliyoorodheshwa hapo juu.

## Mpango wa kutumia njia mbili kwa pamoja

Mpango wa **kutumia njia mbili kwa pamoja** ni mkakati unaolenga kuimarisha ujumuishaji wa ulemavu unaohusisha kutekeleza **programu mahususi za aina fulani za ulemavu** ili kushughulikia mahitaji mahususi na changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu huku ukikuza ujumuishaji wa masuala ya ulemavu kwa jumla. Kwa kutumia mbinu zote mbili, mashirika yanaweza kushughulikia mahitaji ya kipekee ya watu wenye ulemavu huku pia yakihakikisha kuwa ulemavu unajumuishwa katika vipengele vyote vya kazi zao. Programu mahususi za ulemavu zinaweza kujumuisha kutoa huduma maalum, utetezi, na shughuli za kukuza ufahamu wa masuala mbalimbali.

Katika suala la ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu, mbinu ya kutumia njia mbili kwa pamoja inaweza kutumika, kwa mfano, katika kuwajumuisha watu wenye ulemavu ndani ya programu zilizopo tayari za kutoa mafunzo kuhusu usalama na ulinzi, huku kukibuniwa programu maalum za kutoa mafunzo zinazolenga tu mashirika ya watu wenye ulemavu pekee ili kushughulikia mahitaji yao maalum ya usalama. Kwa njia hii, mashirika yanaweza kukuza ujumuishaji kwa jumla na pia ujumuishaji mahususi wa aina tofauti za ulemavu.

## Programu, miradi na bajeti zinazojumuisha ulemavu

Mashirika ya haki za binadamu yanafaa kujumuisha masuala ya ulemavu katika mifumo yao ya kimkakati na kuakisi ushirikishwaji wa ulemavu katika programu zao, miradi na bajeti. Kila hatua muhimu ya **mchakato wa maendeleo ya mradi** (ikiwa ni pamoja na kubuni, utekelezaji, ukusanyaji wa habari, na ufuatiliaji wa kutathmini ubora) inapaswa kuhusisha watu wenye ulemavu, si tu kama 'kundi lengwa' lakini kama mhusika mkuu katika kufanya maamuzi.

Ni muhimu vile vile kuzingatia **upangaji wa bajeti unaojumuisha ulemavu**, mchakato ambao unazingatia mahitaji na vipaumbele vya watu wenye ulemavu, kuhakikisha kwamba mgao wa bajeti unafanywa kwa njia ya kusaidia ushirikishwaji wao na ushiriki kamili katika jamii. Kwa bahati mbaya, mara nyingi bajeti ya ulemavu huchukuliwa au kuonekana, japo kimakosa, kuwa ni ghali. Hata hivyo, ikiwa miradi inalenga kujumuisha ulemavu tangia mwanzo, mchakato huwa rahisi na wa gharama nafuu zaidi. Hapa tunapendekeza baadhi ya mambo ya kufanya ili kutekeleza bajeti zinazojumuisha ulemavu zaidi:

- Panga bajeti **kulingana na tathmini ya mahitaji ya ulemavu jumuishi** ambayo hubainisha mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu katika miradi.
- **Tenga fedha mahususi katika bajeti** ili kutumiwa kwa ajili ya kujumuisha watu wenye ulemavu. Kati ya asilimia 10 hadi 15 ya gharama zinapaswa kuongezwa kwa shughuli muhimu (kama vile vikao vya mafunzo, vitendo vya utetezi, kuchapisha hati au ripoti) ili kuhakikisha kwamba mahitaji kamili na yanayofaa yanazingatiwa. Gharama hizi ni halali kabisa na ni nadra sana kupunguzwa na wafadhili.
- **Kuwashirikisha watu wenye ulemavu katika mchakato wa kupanga bajeti** katika kila awamu, ikiwemo mashauriano kuhusu bajeti, kufanya maamuzi na ufuatiliaji katika utekelezaji.
- Kuhakikisha **uwazi katika bajeti**, kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata taarifa kuhusu bajeti na wanaweza kushiriki katika mchakato huo.

## Kukusanya na kupanga taarifa kuhusu ulemavu

**Kukusanya na kupanga taarifa kuhusu ulemavu** katika programu na miradi kunaweza kusaidia mashirika katika mambo kadhaa kama vile:

- **Kubainisha mahitaji ya watu wenye ulemavu** katika shirika au jamii, kama vile aina za ulemavu, kiwango cha upatikanaji wa huduma na miundombinu, na kiwango cha ubaguzi au unyanyapaa wanaokabiliana nao.
- **Kufuatilia hatua zinazopigwa kuelekea ushirikishwaji kamili wa ulemavu** ikiwa ni pamoja na kuangalia kama mgao wa bajeti unatumika kusaidia katika ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu katika jamii.
- **Kuhakikisha uwajibikaji** - kuhakikisha serikali, mashirika, na washikadau wengine husika wanawajibika katika kutekeleza majukumu na ahadi zao za kuimarisha ushirikishwaji wa walemavu.
- **Kutoa taarifa sahihi na muhimu katika maamuzi ya kisera na kiprogramu** ili kuhakikisha kwamba mahitaji ya watu wenye ulemavu yanatambuliwa na vikwazo vinashughulikiwa na kuondolewa.

Kama mfano wa jinsi ya kukusanya taarifa kuhusu ulemavu, Shirika la the Washington Group on Disability Statistics (2019) lilitengeneza maswali sita yanayojulikana kama **Washington Group Short Set of Questions on Functioning (WG-SS).** Maswali haya ni zana ya wastani, inayotambulika kimataifa ili kutathmini kuenea kwa ulemavu katika jamii.

Maswali hayo ni muhimu kwa ujumuishaji wa ulemavu na uandaaji wa programu kwa sababu yanatoa njia thabiti na linganifu ya kupima ulemavu katika mazingira tofauti, ambayo inaweza kutumiwa katika maamuzi ya kuunda na kutekeleza sera, programu, na huduma ambazo zinajumuisha watu wenye ulemavu. Maswali haya pia ni muhimu katika kutambua na kushughulikia vikwazo vya ushiriki kamili na ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu katika jamii.

## Mawasiliano jumuishi

Sehemu hii inaangazia mbinu na mitindo ya mawasiliano jumuishi, ikiwemo hatua za kuwezesha watu kuwasiliana mtandaoni na matumizi ya majukwaa ya kidijitali.

Kwa bahati mbaya, sio majukwaa yote ya mtandaoni/kidijitali ambayo yanaweza kutumiwa kwa urahisi na watu wenye ulemavu. Mtetezi mmoja mwenye ulemavu alisema, "vifaa na zana za ufikikaji ni kizuizi cha kutimiza ujumuishaji katika mifumo ya kidijitali. Ikiwa hauna simu au kompyuta ambayo inaweza kutumia programu hiyo mahususi, basi hauwezi hata kufikia na kutumia mifumo ya kidijitali''. Mhusika mmoja alisema,

> ***tunapowasiliana mtandaoni, tunahitaji kuhakikisha kwamba kila mtu anayehusika anaweza kupata taarifa. Kwa hivyo, labda tunahitaji kukusanya taarifa kuhusu watu wenyewe kwanza. Kabla ya kuwasiliana na wengine, unaweza kugundua kuwa kuna aina tofauti za ulemavu za kutiliwa maanani. Ikiwa kuna kiziwi anayehitaji kupokea habari hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba kuna mtafsiri wa lugha ya ishara. Ikiwa mtu ana udhaifu wa kuona, unafaa kujua iwapo kifaa anachotumia kimewekwa programu muhimu ya kusoma maneno kwa sauti ili kuwezesha kuwepo kwa mawasiliano yenye ufanisi.***

Mhusika mwingine alisema kuwa "ni muhimu kutathmini mapema mahitaji ya ufikiksaji kwa sababu, mara nyingi, mashirika hushughulikia tu masuala wakati tayari tuko kwenye kikao na watu hukosa kushiriki kikamilifu. Inapendekezwa kutuma fomu mapema na kuwauliza watu "una hitaji lolote la ulemavu?" badala ya kudhania au kuamua bila kufanya hivyo.

Hivi ni baadhi ya vidokezo muhimu vya kuzingatia katika mawasiliano ya mtandaoni ili kuhakikisha ujumuishaji wa watetezi wenye ulemavu:

- **Tumia majukwaa yanayozingatia ufikikaji**: kuna majukwaa kadhaa ya mawasiliano ambayo yanaweza kutumika kuwezesha mawasiliano ya mtandaoni kwa watu wenye ulemavu, kama vile programu za kusoma kwa sauti maneno yaliyopo kwenye skrini, lugha ya ishara kupitia usaidizi wa video na programu inayobadilisha sauti na kuifanya kuwa maandishi yanayoweza kusomwa.
- **Tovuti zinazoangazia ufikikaji**: tovuti zinapaswa kuundwa kwa kuzingatia ufikikaji, kama vile kuwepo kwa maandishi mbadala yanayoelezea picha zilizopo, kuhakikisha kwamba taarifa zinapatikana kwa urahisi pale mtu anapotumia 'keyboard' ya kompyuta, na kuzuia picha zinazowaka kwa haraka ambazo zinaweza kusababisha kifafa au mshtuko wa moyo.
- **Hati zinazozingatia ufikikaji**: Hati zozote zinazowekwa mtandaoni, kama vile ripoti au maelezo ya mikutano, zinapaswa kufanywa ziwe rahisi kupatikana na kueleweka na watu wenye ulemavu, kama vile kutoa maandishi mbadala ya picha, kwa kutumia maandishi yenye ukubwa na mpangilio unaofaa, na kuhakikisha kwamba mtu anaweza kudurusu hati hizo kwa urahisi kwa kutumia 'keyboard' ya kompyuta. Miundo ya **PDF na miundo mingine inaweza kukosa kusomeka kwa urahisi na programu za kusoma skrini**. Unaweza kujaribu kutumia mfumo wa HTML au miundo mingine ambayo inaweza kusomeka kwa urahisi.
- **Tumia maandishi mbadala kwa picha**: maandishi mbadala ni maelezo mafupi ya picha ambayo yanaweza kusomwa kwa sauti na visoma skrini. Hii hutoa fursa kwa watu wenye udhaifu wa kutoona kuelewa picha hizo.

- **Tumia maandishi yenye ukubwa unaofaa na rangi tofauti**: tumia maandishi yenye rangi na ukubwa ambao ni rahisi kusoma na kutofautisha na pia usitumie maandishi ambayo ni madogo sana au membamba sana kuonekana. Rangi ambazo ni rahisi kutofautisha hutoa fursa kwa watu walio na udhaifu wa kuona kusoma maandishi kwenye skrini.
- **Weka nukuu na maelezo ya sauti**: haya hutoa fursa kwa watu wenye udhaifu katika kusikia kufuatilia mazungumzo, video na mikutano mtandaoni. Pia huwanufaisha watu ambao huenda wakakosa uwezo wa kuwasha sauti au wanaozungumza lugha tofauti.
- **Tumia lugha rahisi na wazi**: tumia lugha rahisi na fasaha ili kuhakikisha kuwa taarifa zinaeleweka kwa urahisi na wasomaji wote.
- **Epuka lugha inayokandamiza**: tumia lugha ambayo inalenga kuzungumza na mtu kibinafsi, epuka maneno ya dharau, na kutumia ulemavu kama sitiari.

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba sio zana na vipengele vyote katika programu vinavyoweza kutumiwa na watu wote wenye ulemavu, na kwamba marekebisho ya ziada yanaweza kuhitajika ili kuhakikisha matumizi kamili na kila mtu.

## Kuahidi na kujitolea kutekeleza ufikikaji wa kina kwa wote na muundo wa jumla

**Upatikanaji wa kina wa huduma, bidhaa na muundo wa jumla kwa wote** unalenga kuondoa vizuizi katika jamii na kupanua ufikikaji kwa watu wenye ulemavu. Inamaanisha kutambua na kushughulikia vizuizi katika jamii vinavyozuia ushiriki wa watu wenye ulemavu katika uanaharakati, kama vile vilivyoelezwa katika Sehemu ya 2.3.3.

Hatua moja ya kuelekea kutimiza upatikanaji wa jumla wa huduma na bidhaa kwa wote ni **kufanya ukaguzi** kwa ushirikiano na watetezi wenye ulemavu na mashirika wanayowakilisha ili kutambua mbinu na vikwazo vinavyoweza kuwatenga watu wenye ulemavu. Ukaguzi huo unaweza kuchunguza mazingira yalivyojengwa, kubainisha vizuizi kama vile upana mdogo wa milango, ngazi zisizo na vifaa vya kushikiliwa na mikono, na vyoo visivyoweza kutumiwa na watu wenye ulemavu. Ukaguzi huo unaweza pia kutathmini taarifa za kidijitali kuhusu ufikikaji, kama vile tovuti au hati za kielektroniki, au kuwepo au kutokuwepo kwa visoma skrini na kudurusu kwa kutumia 'keyboard' ya kompyuta pekee. Mashirika yanaweza pia kupitisha na kutekeleza kanuni za muundo wa jumla wakati wa kuunda programu, miradi, na miundombinu, ili kuhakikisha kuwa zinaweza kutumiwa kwa kiasi kikubwa na watu wote bila kuzingatia umri, ukubwa na uwezo wao.

Dhana muhimu ya kutathmini hatua zilizopigwa katika upatikanaji wa jumla wa huduma na bidhaa ni **ukaribu wa ufikikaji** uliopendekezwa na Mia Mingus (2011). Anaelezea hili kama:

> ***hisia ambayo ni ngumu kupatikana, ni ngumu kuelezea wakati mtu mwingine "anaelewa" mahitaji yako ya ufikikaji. Aina ya faraja ambayo mtu mwenye ulemavu anahisi anapokuwa katika kiwango sawa cha ufikikaji na mtu. Wakati mwingine hili linaweza kutokea ukiwa na watu ambao huwafahamu, wawe na ulemavu au la, au wakati mwingine linaweza kutokea kupitia uhusiano unaojengwa kwa miaka mingi.  Linaweza pia kuwa jinsi mwili wako unavyotulia na kisha unafungua roho yako kwa mtu wakati ambapo mahitaji yako yote ya ufikikaji yanatimizwa. Haitegemei pale ambapo mtu anapokuwa na uelewa wa kisiasa wa ulemavu, dhana zinazokandamiza au ufikikaji. Baadhi ya watu ambao nimehisi nao ufikikaji kwa ukaribu zaidi (hasa watu wasiokuwa na ulemavu) ni watu ambao hawana elimu au uelewa wa kisiasa kuhusu ulemavu.***

Kwa hivyo, kiashirio kwamba ufikikaji wa kina umetekelezwa ni wakati watetezi wenye ulemavu wanahisi wamekaribishwa, wamestarehe, wametulia, kuna uwazi, wamehusiana na wengine, na pia kuhusishwa katika nafasi wanazoshiriki.

## Kufadhili watetezi wenye ulemavu na kuwajumuisha katika harakati za haki za binadamu

Wafadhili wana jukumu muhimu katika kusaidia watetezi wenye ulemavu katika kazi zao, na katika kutetea na kusaidia mashirika na harakati za haki za binadamu katika utekelezaji wa kanuni na hatua zinazojumuisha suala la ulemavu. Washiriki katika utafiti huu walitueleza changamoto wanazopata katika kutafuta ufadhili. Mmoja alisema, "Kati ya mamilioni ya dola ambayo hutolewa kwa watetezi wa haki za binadamu, ni kiasi gani hutengwa kwa wale wenye ulemavu? Sijawahi kusikia kuhusu ufadhili wowote unaopatikana kwa watetezi wenye ulemavu". Mada nzito iliyoibuka ni kwamba watu wenye ulemavu wanapaswa kushirikishwa katika michakato ya kufanya maamuzi ndani ya miradi inayohusiana na ulemavu. Kama mshiriki mmoja alivyosema,

> ***yeyote anayekaa kwenye kamati za ufadhili... huamua ni wapi pesa ziende na wapi pesa hizo zitatumika. [Mtu mwenye ulemavu] anaweza kujua kama kuna hitaji maalum la jambo fulani, na ni nini hasa kinachohitaji kufadhiliwa kwa ajili ya hilo. Mbinu hii ni bora zaidi kuliko kuwa na mtu wa nje anayeamua ni wapi fedha zitapelekwa... Kwa hivyo, washirikishe watetezi wa haki za binadamu katika michakato ya kufanya maamuzi.***

Watetezi wenye ulemavu pia walizungumza kuhusu umuhimu wa upatikanaji wa ufadhili, unaoweza kubadilishwa kulingana na mahitaji kutoka kwa wafadhili ambao wanaelewa kwamba mabadiliko hayo yanaweza kutokea.

Pia walitamani wangepata fursa za kushawishi kanuni za ufadhili, na kuhakikisha kuwa fedha zinatolewa mahususi kwa ajili ya watetezi wenye ulemavu.

Jukwaa la Walemavu na Uhisani huwasaidia wafadhili katika kukomesha ukandamizaji uliofanywa kuwa kawaida katika jamii kwa kuongeza ufadhili wa ujumuishaji na haki kwa watu wenye ulemavu. Wanahimiza wakfu na mashirika ya uhisani kushiriki katika **Ahadi yao ya Ujumuishaji wa Ulemavu**, ambayo inatoa ahadi katika maeneo manane ya kazi: ushiriki wa jamii ya watu wenye ulemavu; lugha jumuishi katika masuala ya ulemavu; matukio jumuishi; ukaguzi na mipango jumuishi; utoaji mafunzo na ushiriki wa wafanyakazi; mafunzo na ushiriki wa bodi; utoaji wa ruzuku ya masuala ya ulemavu; na kutathmini utekelezaji na kutoa taarifa. Wanapendekeza vidokezo vifuatavyo kwa wafadhili (Jukwaa la Walemavu na Uhisani, 2023):

- Kuzindua jamii inayohusu kanuni, inayojumuisha wafanyakazi ambao wana nia na ujuzi kuhusu masuala ya ulemavu, ili kukuza mafunzo ya watu wa matabaka sawa na kushauri kanuni za kitaasisi.
- Kutathmini na kupangilia shughuli za ujumuishaji wa ulemavu kuwiana na eneo moja au zaidi za kutoa ufadhili na ruzuku, ili kutambua njia za kusaidia watu ambao wanapokea ufadhili kwa sasa na wale wapya wanaojibidiisha kutatua changamoto ya ukosefu wa usawa katika masuala ya ulemavu.
- Jifunze kutokana na utafiti unaozingatia haki za watu wenye ulemavu
- Jiunge na hazina shirikishi ya haki ya watu wenye ulemavu ili kuendeleza haki za watu wenye ulemavu
- Tengeneza mkakati wa muda mrefu ambao utatumiwa kutathmini juhudi za ujumuishaji wa watu wenye ulemavu ikiwemo malengo, muda wa utekelezaji na timu itakayofanya kazi hiyo.

- Tambua lengo la ufadhili wa ujumuishaji wa ulemavu ili kuimarisha kazi hii (k.m. asilimia 5% ya ufadhili, au kiasi mahususi cha pesa)
- Ili kujifunza zaidi na kuelewa sekta hii vizuri zaidi, toa ufadhili kwa shirika moja la watu wenye ulemavu linaloshughulikia suala fulani mahususi.
- Husisha watu wenye ulemavu katika mikutano au mijadala ya kimkakati ambapo maamuzi ya ajenda ya programu hufanyika.
- Weka suala la ujumuishaji wa ulemavu katika mipango ya kimkakati ili watu wenye ulemavu wajumuishwe katika mbinu za kutafuta ufadhili kuanzia mwanzo.
- Andaa na pia ufadhili mikutano, na fursa za kujifunza kati ya mashirika ya watu wenye ulemavu na makundi mengine ya haki za binadamu kwa ajili ya wale wanaopokea ufadhili.
- Zindua msururu wa mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu ulemavu na ushirikishwaji, ukizingatia mseto wa masuala ya kiprogramu na utendakazi
- Kagua michakato ya kutoa ufadhili kwa ajili ya ujumuishaji wa masuala ya ulemavu. Je, upatikanaji wa programu ya kuwasilisha maombi ukoje? Je, kuna vigezo vya ufadhili vinavyohusiana na ulemavu? Je, kanuni zinazingatia ulemavu zaidi ya vigezo vya kiafya na matibabu?
- Hakikisha kuwa ujumuishaji wa ulemavu ni kigezo katika kanuni zote na maombi ya mapendekezo ya mradi na masharti ya kutoa ufadhili.
- Kagua mawasiliano yote ili kuhakikisha ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu

Katika taarifa yao kwa wafadhili, *Kusaidia Harakati Jumuishi: Kufadhili Haki za Wanawake Wenye Ulemavu* (Dobson, tarehe haijatajwa), Hazina ya Haki za Walemavu na Wakfu wa Channel zinatoa mwongozo mahususi kuhusu jinsi ya kufadhili mashirika ya wanawake wenye ulemavu.

# » Mapendekezo

Watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu daima wamekuwa sehemu muhimu ya mapambano ya kutetea haki za binadamu duniani kote. Hata hivyo, mfumo wa ukandamizaji uliofanywa kuwa kawaida wa kutathmini uwezo na thamani ya watu kulingana na vigezo fulani hutathmini jinsi wao, na watu wengine wenye ulemavu, wanavyochukuliwa katika jamii. Mtazamo wa mfumo huo wa ukandamizaji kuhusu utetezi wa haki za binadamu umeathiri jinsi mchango wa watetezi hao unavyoeleweka katika harakati za kutoa hamasisho kuhusu changamoto na hatari zao. Mwongozo huu unaangazia njia madhubuti ambazo usalama na ulinzi wa watetezi wenye ulemavu unaweza kuimarishwa, jambo ambalo linahitaji ujumuishaji wa kina katika harakati za haki za binadamu. Hii ni safari tegemezi inayohitaji kujitolea kwa pamoja, kujifunza, na mapambano kutoka kwa sekta zote katika harakati za haki za binadamu; ni safari ya lazima na muhimu inayolenga kuwepo kwa jamii yenye haki na usawa na inayozingatia hadhi ya watu wote.

# Marejeleo


- Accenture (2018) *Kufikia usawa: Faida za ujumuishaji wa ulemavu*. Accenture.
- Barry, J., & Đorđević, J. (2007). Kuna haja gani ya mapinduzi iwapo hatuwezi kucheza? Boulder, CO: Hazina ya Hatua za Haraka kwa Haki za Wanawake.
- Barry, J., & Nainar, V. (2008). Mikakati ya usalama ya watetezi wa haki za binadamu wanawake: Sisitiza, pinga, shikilia, kuwepo. Ottawa: Hazina ya Hatua za Haraka kwa Haki za Wanawake; Kvinna Till Kvinna; Watetezi wa Mstari wa mbele.
- Bennett, K., Ingleton, D., Nah, A. M., & Savage, J. (2015). **Mitazamo muhimu kuhusu usalama na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu.** *Jarida la Kimataifa la Haki za Binadamu*, 19(7), 883–895.
- Berne, P. (2015) *Haki za ulemavu – rasimu.* [Mtandaoni] [Ilisomwa 22 Desemba 2023].
- CIVICUS (2023) *Ufuatiliaji wa kiraia: Matokeo ya ulimwengu 2023*. [Mtandaoni] [Ilisomwa 22 Desemba 2023].
- Cohen, J. (haina tarehe) *Itifaki za ulemavu: Vigezo vya kushirikiana na watu wenye ulemavu*. New York: Muungano wa Askari Wastaafu wa Mashariki Waliopooza.
- DefendDefenders (2022) Kupuuzwa na kutoonekana: Watetezi wa haki za binadamu wenye ulemavu katika nchi zenye migogoro, Ethiopia, Somalia, na Sudan Kusini, Kampala: DefendDefenders.
- Degener, T. (2017) Mfumo mpya wa haki za binadamu wenye ulemavu. Katika V. Della Finna, R. Cera, na G. Palmisano (wahariri.), *Makubaliano ya Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu: Maoni.* Springer Cham, kurasa. 41-59.
- Jukwaa la Ulemavu na Ufadhili (2023) *Weka ahadi: Jiunge nasi katika safari ya kutimiza ujumuishaji wa ulemavu.* [Mtandaoni] [Ilisomwa 22 Desemba 2023].
- Dobson, C. (haina tarehe) *Kusaidia harakati za ujumuishaji: Kufadhili haki za wanawake wenye ulemavu*. Hazina ya Haki za Ulemavu na Wakfu wa Channel.
- Durgun, S. (2023) *Utetezi usio wa moja kwa moja: Mbinu ya mageuzi ya chini kwa chini.* 1 Julai. [Mtandaoni] [Ilisomwa22 Desemba 2023].
- Forst, M. (2019) Hali ya watetezi wa haki za binadamu wanawake: *Ripoti ya mwandishi maalum kuhusu hali ya watetezi wa haki za binadamu*. 10 Januari (**A/HRC/40/60**).
- Forst, M. (2016) Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu (2016) *Ripoti ya Mwandishi Maalum kuhusu hali ya watetezi wa haki za binadamu*. 1 Februari (**A/HRC/31/55**).
- Muungano wa Kimataifa wa Walemavu (2020) *Wanazidi kushauriwa, lakini bado hawashiriki: Utafiti wa IDA duniani kuhusu kushiriki kwa mashirika ya watu wenye ulemavu katika kutengeneza programu na sera, 2020*. Muungano wa Kimataifa wa Walemavu
- Lawlor, M. na Quinn, G. (2022) *Taarifa ya pamoja: Watetezi wa Haki za Binadamu wenye ulemavu wanalengwa na kutengwa duniani kote, waonya wataalamu wa Umoja wa Mataifa*. Taarifa ya pamoja ya Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu na Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu hali ya watetezi wa haki za binadamu. Taratibu Maalum za Haki za Kibinadamu za Umoja wa Mataifa. 29 Novemba.
- Shirika la Human Rights Watch (2022), *"Ilikuwa vigumu sana kujilinda": Athari ya mgogoro wa kivita nchini Syria kwa watoto wenye ulemavu*. Shirika la Human Rights Watch.

- Lewis, T.A. (2022) ***Maelezo kuhusu mfumo wa ukandamizaji uliofanywa kuwa kawaida wa kutathmini uwezo na thamani ya watu kulingana na vigezo fulani – Toleo la Januari 2022.*** Talila A. Lewis, 1 Januari. [Mtandaoni] [Ilisomwa 22 Desemba 2023].
- Mingus, M. (2011) ***Ufikikaji wa karibu: kiungo kinachokosekana***, Leaving Evidence, 5 Mei. [Mtandaoni] [Ilisomwa 22 Desemba 2023].
- Nah, A.M. (2021) ***Kukabili uzima wa kimwili na hisia katika aina hatari za utetezi wa haki za binadamu***, *Social Movement Studies*, 20:1, 20-35
- Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Kibinadamu (2006) *Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu*. 12 Desemba (**A/RES/61/106**).
- Oliver, M. (1996) ***Kuelewa ulemavu: Kuanzia nadharia hadi utendaji***, New York: Chapa ya St Martin.
- Sins Invalid (haina tarehe) ***Kanuni 10 za haki za ulemavu.*** [Mtandaoni] [Ilisomwa 22 Desemba 2023].
- Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Watu Wenye Ulemavu (2018) *Maoni ya Jumla Na. 7 (2018) kuhusu ushiriki wa watu wenye ulemavu, wakiwemo watoto wenye ulemavu, kupitia mashirika yanayowawakilisha, katika utekelezaji na ufuatiliaji wa Mkataba.* 9 Novemba (**CRPD/C/GC/7**).
- Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (1999) *Azimio lililopitishwa na Baraza Kuu: Tamko la Haki na Wajibu wa Watu Binafsi, Vikundi na Vyombo vya Jamii Kukuza na Kulinda Haki za Binadamu za Msingi Zinazotambuliwa kote Ulimwenguni*, 8 Machi (**A/RES/53/144**).
- Idara ya Umoja wa Mataifa ya Masuala ya Kiuchumi na Kijamii (2023) ***Mwongozo wa kanuni za Mkataba.*** [Mtandaoni] [Ilisomwa 22 Desemba 2023].
- Hazina ya Watoto ya Umoja wa Mataifa (2022) ***Sera na mkakati wa ujumuishaji wa ulemavu 2022-2030***. New York: UNICEF.
- Shirika la Washington Group on Disability Statistics (2019) ***Kuelewa na kutumia Maswali ya shirika la Washington Group kuhusu Ulemavu.*** [Mtandaoni] [Ilisomwa 22 Desemba 2023].
- Shirika la Afya Duniani (2023) ***Ulemavu***. 7 Machi. [Mtandaoni] [Ilisomwa 22 Desemba 2023].
- Shirika la Afya Duniani (2022) ***Ripoti ya dunia kuhusu usawa na haki za kiafya kwa watu wenye ulemavu: Muhtasari***. Geneva: Shirika la Afya Duniani.
- Shirika la Afya Duniani (2002) ***Kuelekea katika kuwa na lugha ya pamoja ya utendaji, ulemavu na afya, ICF***. Geneva: WHO, WHO/EIP/GPE/CAS/01.3.


FIGHT POVERTY
NOT THE POOR
A Living
Wage
for All
End
Povert
Nov


End
Now!

# Kuimarisha Ujumuishaji, Ulinzi na Ustawi wa Watetezi wa Haki za Binadamu wenye Ulemavu

